# UCHUMI WETU

TOLEO NA. 04, APRILI 2026

BENKI KUU YA TANZANIA
1966-2026











# NENO LA GAVANA



**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Kama ilivyo ada, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) hutoa jarida lake la UCHUMI WETU  kila robo mwaka, linalowapa taarifa na uelewa wa masuala mbalimbali ya uchumi na sera za fedha yanayotekelezwa na taasisi za fedha ndani na nje ya nchi yetu. Ninayo furaha ya kuwakaribisha wasomaji wote katika toleo hili la nne.

Kabla ya kugusia machache yaliyomo kwenye jarida hili, napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa miongozo mbalimbali yenye lengo la kuendelea kuinua uchumi wa nchi yetu, hususan katika kutimiza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Vilevile, natumia nafasi hii kutoa salamu za pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wadau wa BoT kwa kuondokewa na magavana wastaafu wawili katika kipindi kifupi. Hakika hili ni pigo kubwa kwetu. Tarehe 19 Januari 2026, tulimpoteza Gavana wa kwanza wa BoT, Hayati Edwin Mtei ambaye alihudumu katika wadhifa huo kuanzia mwaka 1966 hadi 1974. Aidha, tarehe 13 Machi 2026, tulimpoteza aliyekuwa Gavana wa nne wa BoT, Dkt. Idris Rashid. Tunawaombea wapumzike kwa amani.

Mbali na misiba hiyo, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2026, BoT tulimuaga aliyekuwa Naibu Gavana Utawala na Udhibiti wa Ndani, Bw. Julian Banzi Raphael na kumkaribisha Naibu Gavana mpya, Dkt. Rahma Mahfoudh. Tunamshukuru Bw. Banzi kwa utumishi wake uliotukuka na tunamtakia maisha mema ya ustaafu wa shughuli za Serikali. Aidha, tunampongeza Dkt, Mahfoudh kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kumtakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yake. Tunaahidi kumpa ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yake.

Ndugu msomaji wetu, katika kutathmini mwenendo wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2026, kuna viashiria kwamba mwenendo wa ukuaji wa uchumi unaweza kuathiriwa na mgogoro wa kisiasa Mashariki ya Kati, ulioanza mwezi Februari 2026, hali inayovuruga mnyororo wa ugavi na kusababisha ongezeko la bei za bidhaa duniani. Vilevile, mfumuko wa bei unaweza kuongezeka katika nchi nyingi, kutokana na kupanda kwa bei za nishati na ongezeko la gharama za usafirishaji.

Kwa upande wa Tanzania, tunategemea kwamba uchumi utakua kwa asilimia 6.3 mwaka huu wa 2026. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, ukuaji wa uchumi kwa Tanzania Bara unakadiriwa kufikia asilimia 6.2 na asilimia 6.7 kwa Zanzibar. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, huduma za fedha na bima, pamoja na utalii. Katika robo ya pili ya mwaka 2026, uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.1 na asilimia 6.6, mtawalia. Hata hivyo, kuendelea kwa mgogoro ya Mashariki ya Kati kwa muda mrefu kunaweza kupunguza matarajio ya kasi hii ya ukuaji wa uchumi.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa ndani ya lengo la kati ya asilimia 3 hadi 5, ambapo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2026, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.3 kwa Tanzania Bara na asilimia 4.5 kwa Zanzibar. Hii ni kutokana na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha pamoja na utulivu wa bei za chakula na nishati. Changamoto ya kupanda kwa bei za nishati na usafirishaji duniani zinaweza kupunguzwa kwa kiasi utulivu wa bei za bidhaa mbalimbali nchini na uthabiti wa thamani ya shilingi. Hata hivyo, tunatarajia kwamba mfumuko wa bei utaendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5.

Sekta ya benki imeendelea kuwa thabiti, ikiwa na ukwasi wa kutosha na mtaji unaoweza kuhimili vihatarishi. Ubora wa mikopo umeendelea kuimarika kutokana na mazingira wezeshi ya biashara na usimamizi madhubuti wa vihatarishi, ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulikuwa asilimia 2.9 mwezi Februari 2026, ndani ya kiwango kinachovumilika cha asilimia 5. Mifumo ya malipo pia imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi.

Urari wa malipo ya kawaida uliendelea kuimarika, ambapo unakadiriwa kufikia nakisi ya asilimia 2.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka unaoishia Machi 2026, kutoka asilimia 2.4 mwaka 2025, licha ya kuongezeka kwa migogoro ya kisiasa duniani. Mwenendo huu umetokana na ongezeko la mauzo ya nje ya nchi, hususan dhahabu, utalii na mazao ya kilimo.

Ndugu msomaji wetu, katika toleo hili la nne la Jarida la UCHUMI WETU, tunakukaribisha kupata maarifa kuhusu masuala muhimu yanayohusu uchumi wa Taifa letu. Miongoni mwa habari zilizomo katika toleo hili ni pamoja na programu ya ununuzi wa dhahabu, ambapo utaelezwa dhima yake, utekelezaji wake, na mchango wake katika kuimarisha akiba ya nchi ya fedha za kigeni. Aidha, Jarida hili linafafanua mfumo wa kisheria unaoipa Benki Kuu mamlaka ya kusimamia na kutunza akiba ya nchi ya fedha za kigeni, ikiwemo dhahabu, jambo ambalo ni mhimili muhimu katika kudumisha uthabiti wa uchumi wa nchi yetu.

Kadhalika, kuelekea katika kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Benki Kuu, yatakayofanyika tarehe 12 Juni 2026, Jarida hili linaeleza mipango ya Benki Kuu katika kutumia tukio hilo muhimu kama fursa ya kukutana na wadau mbalimbali, kutoa elimu ya fedha, na kuongeza uelewa wa majukumu ya Benki Kuu katika kukuza uchumi jumuishi na endelevu.

Katika toleo hili pia, utapata fursa ya kujifunza kuhusu umuhimu wa mifumo ya malipo katika kuchochea ukuaji wa uchumi, ambapo kwa Tanzania mifumo yote ya malipo imeendelea kuwa salama na thabiti.

Kwa kuhitimisha, napenda kukukaribisha tena msomaji wetu katika toleo hili la nne la Jarida la UCHUMI WETU. Nina imani kuwa kupitia makala na habari mbalimbali zilizomo kwenye jarida hili, utapata maarifa na uelewa utakaosaidia katika kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Nawatakia wote usomaji mwema.

**Emmanuel Mpawe Tutuba**
Gavana, Benki Kuu ya Tanzania.

# MEZA YA MHARIRI MKUU



***Ndugu Msomaji wetu,***

Ni wakati mwingine tena nakukaribisha katika Jarida la UCHUMI WETU toleo la nne. Jarida hili linalenga kukuongezea uelewa na kukupatia taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya uchumi na sekta ya fedha nchini, hususan yale yanayoratibiwa na kusimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa sheria.

Katika toleo hili, utapata maelezo ya kina kuhusu shughuli na majukumu ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika kusimamia na kuratibu uthabiti wa sekta ya fedha pamoja na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Miongoni mwa habari tulizokuandalia katika toleo hili ni pamoja na maelezo ya kina kutoka kwa Gavana wa Benki Kuu kuhusu dhana ya ununuzi wa dhahabu, umuhimu wake katika kuimarisha akiba ya Taifa, pamoja na sheria inayoipa Benki Kuu mamlaka ya kutunza akiba ya Taifa kupitia njia mbalimbali ikiwemo dhahabu na fedha za kigeni. Vilevile, utapata uelewa mpana kuhusu nafasi ya mifumo ya malipo ya Taifa katika kuwezesha ulipaji wa miamala kwa ufanisi, usalama na kwa wakati.

Kwa kushirikiana na wadau wetu mbalimbali, utapata fursa ya kupata habari na taarifa kutoka kwa taasisi za fedha nchini ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Mitaji na Dhamana (CMSA), Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

Katika kuendeleza ushirikiano na jamii inayotuzunguka, Benki Kuu imeendelea kushiriki katika shughuli za kijamii kwa kuwafikia makundi mbalimbali. Katika mwezi mtukufu wa Ramadhan, Benki Kuu kupitia makao makuu na matawi yake yote ilifanikiwa kuandaa futari na kutoa misaada kwa wahitaji, ikiwa ni sehemu ya kuimarisha mshikamano wa kijamii.

Aidha, Benki imeendelea kutoa elimu kwa umma na makundi maalumu kuhusu majukumu yake pamoja na umuhimu wa utunzaji sahihi wa fedha ili ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Ni matumaini yangu kuwa kupitia jarida hili, utapata fursa ya kuelewa kwa kina masuala ya uchumi na fedha kupitia makala, vibonzo, habari, shairi, picha na maudhui mbalimbali yaliyomo katika toleo hili la nne la UCHUMI WETU.

Endapo una maoni, ushauri au mapendekezo yoyote, tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe: ***botcommunications@bot.go.tz***

Nakutakia usomaji mwema.

***Victoria Msina***
Meneja Mawasiliano
Benki Kuu ya Tanzania.

# RIBA YA BENKI KUU YASALIA ASILIMIA 5.75 ROBO YA PILI 2026

Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeamua kuendelea na kiwango cha Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate - CBR) cha asilimia 5.75 kwa robo ya pili ya mwaka 2026, kiwango ambacho kilitumika pia katika robo ya kwanza ya mwaka 2026.

Riba ya Benki Kuu ni kiwango kinachowekwa na BoT kama rejea katika utekelezaji wa shughuli zake mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukopesha benki za biashara. Kiwango hiki huathiri riba za mikopo baina ya benki za biashara, ambazo zinapaswa kuwa ndani ya wigo wa asilimia +/-1.5. ya riba ya Benki Kuu iliyowekwa.

Uamuzi huo ulitangazwa Aprili 2, 2026 na Naibu Gavana anayesimamia Sera za Fedha na Uchumi, Dkt. Yamungu Kayandabila, wakati wa mkutano na viongozi wa benki, taasisi za fedha pamoja na waandishi wa habari.

Akizungumza katika mkutano huo, Dkt. Kayandabila alisema uamuzi wa kubakiza CBR ulifikiwa baada ya tathmini ya kina ya hali ya uchumi wa ndani na wa dunia.

"Kiwango hicho kilionekana ni sahihi kwa sasa katika kudhibiti mfumuko wa bei kubakia ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5".

Aliongeza kuwa kiwango hicho cha riba kitawezesha kupunguza athari za migogoro ya kisiasa ulimwenguni ambayo inaweza kuathiri uchumi nchini.

"Kiwango hicho kitawezesha kupunguza athari za mgogoro wa kisiasa unaoendelea Mashariki ya Kati kwenye uchumi wa nchi yetu. Mgogoro huo umeathiri biashara, uwekezaji, na ustahimilivu wa uchumi wa dunia". Alisema.

Aidha, Dkt. Kayandabila alieleza kuwa kamati imeamua kupunguza wigo wa riba ya Benki Kuu kutoka asilimia +/-2 hadi asilimia +/-1.5, kuanzia mwezi Aprili 2026 kwa lengo la kudhibiti mfumuko wa bei.

"Lengo la hatua hii ni kuboresha ufanisi wa utekelezaji wa sera ya fedha katika kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo na kuchochea ukuaji wa uchumi. Kufuatia uamuzi huu, wigo wa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki utakuwa kati ya asilimia 4.25 hadi asilimia 7.25 kwa robo ya pili ya mwaka 2026". Alisema.

Kuhusu mwenendo wa uchumi wa nchi, Dkt. Kayandabila, alisema mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati unaweza kuwa na athari kubwa katika uchumi wa ndani.

"Hata hivyo, ukuaji wa uchumi umeendelea kuimarika, ambapo katika robo ya kwanza ya mwaka 2026 ukuaji wa uchumi kwa Tanzania Bara unakadiriwa kufikia asilimia 6.2 na asilimia 6.7 kwa Zanzibar. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, huduma za fedha na bima, pamoja na utalii".

Naye, Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki (TBA) ambaye pia ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Citi Bank, Bw. Geofrey Mchangila aliipongeza BoT kwa usimamizi thabiti wa sekta ya fedha na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Alisisitiza usimamizi huo umechangia kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu hadi kufikia asilimia 2.9, kiwango kilicho chini ya ukomo unaovumilika wa asilimia 5, kudumisha utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za kigeni, pamoja na kuwepo kwa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni inayozidi dola za Marekani bilioni 6.2 ambayo inayotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.8 kiwango ambacho kipo juu ya ukomo wa chini wa kisheria wa kuanzia miezi 4.



Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza wakati wa mkutano na viongozi wa benki, taasisi za fedha pamoja na waandishi wa Habari kwa ajili ya kutangaza riba ya Benki Kuu.



Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA), Bw. Geofrey Mchangila, akizungumza wakati wa mkutano na viongozi wa benki, taasisi za fedha pamoja na waandishi wa Habari kwa ajili ya kutangaza riba ya Benki Kuu.





Naibu Gavana wa BoT, Dkt. Yamungu Kayandabila (katikati), akitangaza kiwango cha Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate) kwa robo ya pili ya mwaka wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Dar es Salaam tarehe 2 Aprili 2026. Wengine kutoka kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania, Geofrey Mchangila, Naibu Gavana (Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha) Bi. Sauda Msemo, Naibu Gavana (Utawala na udhibiti wa ndani), Dkt. Rahma Mahfoudh pamoja na Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi, Dkt. Suleiman Missango.

# MUHTASARI WA TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA KWA ROBO YA PILI YA MWAKA 2026

**02 APRILI 2026**

**RIBA YA BENKI KUU KWA ROBO YA PILI YA 2026 KUBAKIA 5.75%**




### UKUAJI WA UCHUMI

Katika robo ya pili ya mwaka 2026, uchumi wa Tanzania bara na Zanzibar unatarajiwa kukua kwa 6.1% na 6.6%, mtawalia.

### MFUMUKO WA BEI

Katika robo ya pili ya mwaka 2026, utaendelea kubaki ndani ya lengo la 3% hadi 5%.

### URARI WA MALIPO YA KAWAIDA

**Tanzania Bara:**

Unakadiriwa kufikia nakisi ya 2.2% ya pato la Taifa kwa mwaka unaoishia Machi 2026, kutoka 2.4% mwaka 2025

### AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI

Imezidi dola za Marekani bilioni 6.2, ikitosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.8.

### SEKTA YA KIBENKI

Uwiano wa mikopo chechefu (NPLs) uliendelea kupungua hadi kufikia 2.9%, chini ya kiwango cha juu linachovumilika cha 5%.

### UTEKELEZAJI WA SERA YA BAJETI

Makusanyo ya kodi yalivuka lengo kutokana na ukuaji wa uchumi, kuimarika kwa usimamizi, na ulipaji wa hiari.

# RAIS SAMIA AWEKA JIWE LA MSINGI MATANKI YA MAFUTA, KUCHOCHEA UCHUMI




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa matanki ya kupokea na kusambaza mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam.

Hafla hiyo ilifanyika Machi 3, 2026 ambapo inatajwa kuwa hatua inayotarajiwa kuimarisha uchumi wa nchi na kuongeza ufanisi katika sekta ya nishati.

Mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) unatajwa kuwa sehemu ya mkakati mpana wa Serikali wa kuboresha miundombinu ya bandari na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Akizungumza wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi jijini Dar es Salaam, Rais Samia alisema; "Mradi huu utasaidia kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi na kusambaza mafuta, jambo hili litaongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati na kuchochea shughuli za kiuchumi,"alisema Rais Samia.

Alieleza kuwa kukamilika kwa matanki hayo kutapunguza changamoto za ucheleweshaji wa meli bandarini pamoja na gharama zinazotokana na kusubiri kushusha shehena za mafuta, hali ambayo kwa sasa imekuwa ikiathiri gharama za bidhaa za mafuta kwa watumiaji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Bw. Bakari Machumu ilieleza kuwa kwa sasa meli za mafuta huchukua wastani wa siku 22 kuhudumiwa bandarini, lakini kukamilika kwa mradi huo kunatarajiwa kupunguza muda huo hadi takribani siku saba kwa kila meli.

"Kupungua kwa muda wa kuhudumia meli kutasaidia kupunguza gharama za tozo za ucheleweshaji ambazo hufikia takribani Dola za Marekani 25,000 kwa siku kwa meli moja,"ilieleza taarifa hiyo.

Mbali na hilo, mradi huo pia utaongeza uwezo wa bandari kupokea na kuhifadhi mafuta kutoka mita za ujazo zaidi ya milioni moja hadi kufikia takribani mita za ujazo milioni 1.43, sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 35.

Ongezeko hilo linatarajiwa kuimarisha akiba ya kimkakati ya mafuta nchini na kusaidia nchi kukabiliana na misukosuko ya soko la mafuta duniani.

Aidha, Serikali imeeleza kuwa kuimarika kwa miundombinu ya bandari kutachochea biashara ya kikanda, kwani Tanzania itakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuhudumia nchi jirani zinazotegemea Bandari ya Dar es Salaam kwa usafirishaji wa bidhaa.

Mradi huo una gharama ya zaidi ya TZS bilioni 701 na ulianza kutekelezwa Agosti 2024, huku ukitarajiwa kukamilika Februari 2027. Utakapokamilika utakuwa na matanki 15 ya kuhifadhi mafuta aina mbalimbali ikiwamo dizeli, petroli na mafuta ya ndege (Jet A1).

# ZANZIBAR YAIMARISHA UHIFADHI WA MAENEO YA KIHISTORIA KUKUZA UCHUMI



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Balozi wa Slovakia nchini Tanzania, Bw. Ivan Lančarič, aliyetembelea Ikulu Zanzibar Aprili 1, 2026.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imeweka mkazo katika kuhifadhi na kuimarisha maeneo ya kihistoria, hatua inayolenga kuchochea ukuaji wa uchumi hususan kupitia sekta ya utalii.

Akizungumzia suala hilo, Rais wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alisema juhudi hizo ni sehemu ya mkakati mpana wa kuongeza mchango wa urithi wa kihistoria katika pato la taifa pamoja na kulinda utamaduni wa visiwa hivyo.

Hayo aliyasema Ikulu Zanzibar Aprili 1, 2026 alipokutana na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Bi. Marjo Crompvoets, Rais Mwinyi alieleza kuwa maboresho yanayoendelea katika jengo la kihistoria la Sinema ya Majestic, lililopo Vuga, ni mfano wa ushirikiano wenye tija kati ya Zanzibar na washirika wa maendeleo.

Alisema jengo hilo linakarabatiwa kwa kuzingatia muonekano wake wa asili, huku likipangwa kutumika kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kiutamaduni, hatua itakayoongeza vivutio vya utalii mijini Unguja.

"Tunatambua mchango wa maeneo ya kihistoria katika kukuza uchumi. Hivyo, tunaendelea kuweka mipango ya muda mrefu ya kuyahifadhi na kuyatumia kama rasilimali ya maendeleo," alisema Rais Mwinyi.

Aidha, alibainisha kuwa Serikali inalenga kuvutia wawekezaji zaidi katika sekta za kimkakati zikiwemo utalii, uvuvi, viwanda na kilimo ili kuongeza ajira na mapato ya taifa.

Kwa upande wake, Balozi Crompvoets aliipongeza Zanzibar kwa hatua kubwa za maendeleo ya kiuchumi, akitaja uwekezaji katika miundombinu kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji huo. Aliahidi kuendelea kuhamasisha wawekezaji kutoka Uholanzi kuangalia fursa zilizopo visiwani humo.

Katika hatua nyingine, Rais Mwinyi alikutana na Balozi wa Slovakia nchini Tanzania, Bw. Ivan Lančarič, ambapo alisisitiza dhamira ya Zanzibar kupanua wigo wa ushirikiano wa kiuchumi na nchi hiyo, hususan katika uwekezaji, biashara na utalii.

Balozi Lančarič alieleza kuwa Slovakia inapanga kufungua ubalozi wake nchini Tanzania, hatua itakayorahisisha ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi kati ya nchi hizo mbili, pamoja na kukuza uwekezaji katika sekta za viwanda na teknolojia.

Hatua hizi zinaashiria dhamira ya Zanzibar kujipambanua kama kitovu cha uwekezaji na utalii katika Ukanda wa Afrika Mashariki, huku ikitumia



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Mhe. Bi. Marjo Crompvoets, aliyetembelea Ikulu Zanzibar Aprili 1, 2026.

# FAHAMU SABABU BOT, KUNUNUA, KUUZA DHAHABU



**Benki Kuu imeendelea kupanga na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza akiba ya fedha za kigeni, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa dhahabu. Mafanikio katika ununuzi wa dhahabu yaliifanya Benki Kuu kupata tuzo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

Je, Unafahamu sababu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kununua dhahabu? Na vipi kuhusu umuhimu wake katika kuimarisha akiba ya fedha za kigeni? Makala hii inafafanua maswali hayo yote kwa kina, tafadhali fuatilia...

Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba katika mahojiano maalumu na jarida hili amesema ununuzi, uhifadhi na uuzaji wa dhahabu ni suala ambalo lipo kisheria hususan katika majukumu ya Benki Kuu.

Akifafanua suala hilo, Gavana Tutuba anasema BoT huifadhi fedha mbalimbali za kigeni katika kuimarisha akiba ya fedha za kigeni ya Taifa ambapo mwaka 2024 mwezi Oktoba rasmi ilianza kununua na kuhifadhi dhahabu kama njia mojawapo ya kuongeza aina ya fedha za kigeni zinazohifadhiwa na BoT.

"Sheria namba nne ya Benki Kuu kifungu cha 5 inaeleza majukumu ya Benki Kuu, ambapo jukumu moja wapo ni kununua, kuhifadhi na kuwekeza akiba ya fedha za kigeni. Kuna aina mbalimbali ya fedha za kigeni kama vile Dola za Marekani, Australia, Yuan, Rand,"anasema Gavana Tutuba.

Akizungumzia kuhusu uuzwaji wa dhahabu hizo, Gavana Tutuba pia anasema ni suala ambalo lipo kisheria; "Lakini pia , kwenye sheria hiyohiyo kifungu cha 51 na 52 kinaeleza wazi kwamba BoT inaweza kununua, kuuza, kuhifadhi dhahabu itakapoona inafaa."

Katika mahojiano hayo yaliyofanyika Februari 2026 alifafanua kuwa sababu ya BoT kuwa na mpango wa kuuza dhahabu ni kuimarisha uwiano wa fedha za kigeni inazozihifadhi, kwani jumla yake lazima ifike asilimia 100, na kwa sasa dhahabu inazidi malengo ya awali.

"Awali wakati tunaanza mpango huu, Oktoba 2024, tuliweka malengo kuwa ndani ya miaka mitatu tuwe na tani 20, lakini mpaka sasa (Februari 2026) ni mwaka mmoja tu lakini tuna tani 19, unaweza kuona ili uwiano uwepo na fedha nyingine za kigeni, lazima dhahabu tuiuze ili tupate nafasi ya kuendelea kununua kwa wachimbaji,"amefafanua Gavana Tutuba.

Mbali na ununuzi wa dhahabu kusaidia uimarishaji wa thamani ya shilingi yetu na akiba ya fedha za kigeni, Gavana Tutuba amesema pia mpango huo umerasimisha soko la dhahabu nchini, na wachimbaji wengi sasa wanauza dhahabu zao BoT.

Akikazia suala hilo la uwekezaji wa fedha za kigeni katika maeneo tofauti (diversification) Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha wa BoT, Bw. Emmanuel Akaro, anasema kuhusu taarifa za kuuza dhahabu, itakayouzwa ni ile iliyozidi kiwango kilichoidhinishwa, kwa lengo la kusawazisha mizania ya akiba ya fedha za kigeni nchini.

"Sababu ya Benki Kuu kuuza dhahabu ni kujitoa kwenye vihatarishi vya kuwekeza kwenye dhahabu peke yake. Lazima tuhakikishe uwiano wa dhahabu na fedha nyingine za kigeni kwenye mizania ya Benki Kuu zinaendana na matarajio ya Bodi, matarajio ya nchi na matarajio ambayo hayatupelekea sisi kupata hasara"

Kuhusu dhahabu kuuzwa na fedha kutumika katika miradi ya kimkakati, Gavana Tutuba anasema kuwa kuna utaratibu wa BoT kuipatia Serikali fedha ikiwamo gawio.

'BoT ni taasisi ya Serikali, hivyo kila mwaka hutoa gawio lake kwa Serikali na hata ikiuza dhahabu basi katika kile kiwango ilichokiingiza itatoa gawio kwa Serikali na sio kufadhili miradi kama inavyodaiwa mitandaoni,' anasema Gavana Tutuba.

Mbali na hilo, kuhusu kuhifadhi dhahabu fedha katika Benki Kuu ya Uingereza, Bw. Akaro ametaja faidha mbalimbali za kuihifadhi katika nchi hiyo ikiwemo ;

'Kuongeza uaminifu wa kifedha wa nchi (Financial Credibility), kinga dhidi ya hatari ya soko la fedha (Hedging Against Currency Risk), uwezo wa kuhamasisha mikopo (Collateral or Swap Tool), kuimarisha urari wa malipo (Balance of Payments Support), uwekezaji wa kimkakati (Strategic Reserve Diversification), Inaweza kuzalisha mapato (Income-Generating Potential) na pia ni mali inayotambulika kimataifa (Globally Recognized Asset),"alisema Bw. Akaro.

# RIPOTI ZETU: DHAHABU KINARA KATIKA MAUZO YA NJE JANUARI 2026



Katika kuendelea kutimiza malengo ya Dira ya Taifa ya Mwaka 2050 inayohamasisha ukuaji mkubwa wa kiuchumi, Dhahabu imekuwa kinara katika mauzo ya nje Januari 2026 kwa asilimia 39.3 ikilinganishwa na kipindi kama hiko mwaka jana.

Kwa mujibu wa takwimu za Ripoti ya Tathmini ya Mwezi Februari 2026 iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaonesha dhahabu imeongoza kwa mauzo ya nje (exports) mwezi huo kwa kuingiza Dola za Marekani Milioni 4,900.7 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 3,517.5 mwezi kama huo 2025.

Kuhusu dhahabu kuongoza katika mauzo ya nje na kuingiza fedha nyingi za kigeni, ripoti hiyo imeeleza kuwa hali hiyo imechangiwa na kuimarika kwa soko la dunia la bidhaa hiyo katika mwezi Januari.

“kwa kiasi kikubwa ongezeko la mauzo ya nje ya dhahabu umechangiwa na kupanda sana kwa bei katika soko la kimataifa pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji,”imefafanua ripoti hiyo.

Mbali na dhahabu, huduma na mazao mengine yaliyoingia fedha nyingi za kigeni Januari 2026 ni pamoja na; Utalii, usafirishaji, bidhaa za viwandani, tumbaku na korosho.

Kwa upande wa utalii uliingiza Dola za Marekani Milioni 3,969.6 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 3,933.7 katika kipindi kama hiko mwaka 2024. Ukifuatiwa na usafirishaji ambao uliingiza Dola za Marekani 2,874.5 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 2,365 katika kipindi kama hiko mwaka jana.

Bidhaa za viwandani Januari 2026 ziliingiza Dola za Marekani 1,702 ikilinganishwa na Dola za Marekani 1,320.5 sawa na ongezeko la asilimia 28.9.

Kwa upande wa zao la tumbaku pia mauzo yake yaliongezeka kutoka Dola za Marekani 539.9 Januari 2025 hadi Dola za Marekani 573.3 Januari 2026.

# MPANGO WA UNUNUZI WA DHAHABU WA BOT WAIVUTIA KENYA





Naibu Gavana wa BoT, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza katika kikao na ujumbe kutoka Benki Kuu ya Kenya kilichofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam, tarehe 13 Januari 2026.

Wakati Benki Kuu ya Tanzania ikiendelea na mpango wa ununuzi wa dhahabu kwa ajili ya kuongeza hifadhi ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi, nchi mbalimbali zimevutiwa na hatua hiyo na kuonesha nia ya kujifunza.

Miongoni mwa nchi hizo ni Kenya, ambapo ujumbe wa wataalamu wake kutoka Benki Kuu ya Kenya (CBK) Januari 13, 2026 ulitembelea BoT Makao Makuu Ndogo jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujifunza zaidi.

Ujumbe huo ulioongozwa na Naibu Gavana wa CBK, Dkt. Susan Koech, ulivutiwa na namna BoT inavyofanya mchakato huo wa ununuzi wa dhahabu.

Wataalamu hao kutoka Kenya walikaribishwa na Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, ambaye aliwaeleza wageni hao kuwa mpango huo unaohusisha ununuzi wa dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo na wakubwa umeleta mafanikio makubwa katika kuongeza hifadhi ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania.

Kwa upande wake, Dkt. Susan Koech, aliishukuru BoT kwa kuwapokea na kuwapa fursa ya kujifunza kuhusu mpango huo, akieleza kuwa BoT imekuwa mfano wa kuigwa katika utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa dhahabu.

“Tumejionea mageuzi makubwa yaliyofanywa na BoT katika mpango wa ununuzi wa dhahabu pamoja na mafanikio yake. Nakumbuka katika mkutano wa Kamati ya Masuala ya Fedha (Monetary Affairs Committee – MAC) unaojumuisha Benki Kuu za nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, BoT ilipewa jukumu la kuzisaidia nchi nyingine katika ukanda huu katika utekelezaji wa mpango huu,” alisema Dkt. Koech.

Kufuatia kuanza kutekelezwa kwa Sheria ya Madini, kifungu cha 59, kuanzia tarehe 1 Oktoba 2024 hadi tarehe 13 Januari 2026, jumla ya tani 17.9168 za dhahabu zenye thamani ya takribani dola za Marekani bilioni 2.44417 zilinunuliwa.

Pia, katika ziara hiyo ujumbe wa CBK ulitembelea ofisi ya Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Mwanza, kiwanda cha kusafisha madini ya dhahabu cha Mwanza Precious Metals Refinery pamoja na kiwanda cha kusafisha madini ya dhahabu cha Geita.



Naibu Gavana wa CBK,Dkt. Susan Koech, akizungumza katika kikao na Naibu Gavana wa BoT, Dkt. Yamungu Kayandabila, kilichofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam, tarehe 13 Januari 2026.



# GAVANA BOT: MIVUTANO YA KISIASA MASHARIKI YA KATI INA ATHARI KIUCHUMI



Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, akizungumza katika kikao na Mkurugenzi wa Benki ya Dunia wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bw. Hassan Zaman, kilichofanyika Machi 30, 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Benki ya Dunia wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bw. Hassan Zaman, akizungumza katika kikao na Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, kilichofanyika Machi 30, 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, amesema mivutano ya kisiasa inayoendelea mashariki ya kati inaweza kuleta athari katika uchumi wa Tanzania na dunia kwa ujumla.

Gavana Tutuba aliyasema hayo Jumatatu Machi 30, 2026 alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Benki ya Dunia wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika anayeshughulikia masuala ya uchumi, sekta ya fedha na utawala bora, Bw. Hassan Zaman.

"Mivutano ya kisiasa inayoendelea Mashariki ya Kati inaweza kuleta athari kwa uchumi wa Tanzania na dunia kwa ujumla hasa katika bei ya mafuta na mnyororo wa ugavi.

"Hata hivyo, mfumuko wa bei nchini kwa robo ya kwanza ya mwaka ulikuwa asilimia 3.3, kiwango ambacho bado kipo ndani ya lengo la kati ya asilimia 3 hadi 5," aliongeza Gavana Tutuba.

Pia, Gavana Tutuba alisisitiza kuwa; "Benki Kuu itaendelea kushirikiana na Serikali katika kufanya tathmini na kuweka sera madhubuti zitakazosaidia uchumi wa nchi usiathirirwe kwa kiasi kikubwa na migogoro hiyo.

Kwa upande wake, Bw. Zaman aliipongeza BoT kwa juhudi zake za kuendelea kusimamia vizuri uchumi wa nchi, hasa katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiuchumi.

Ikumbukwe kuwa mvutano wa kisiasa katika ukanda wa Mashariki ya Kati umechukua sura mpya mwaka 2026 baada ya kuzuka kwa mapigano kati ya Marekani, Israel na Iran, hali iliyochochea kuhusika kwa mataifa mengine ya eneo hilo.

Mgogoro huo, ulianza mwishoni mwa Februari 2026 unatajwa kuwa na athari mbalimbali kiuchumi hususan kupanda kwa bei ya mafuta na ucheleweshaji wa mizigo na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji.

# GAVANA MSTAAFU PROF. LUOGA AIMWAGIA MAUA MAKUMBUSHO YA BOT




Gavana, Bw. Emmanuel Tutuba, akimkabidhi zawadi ya ramani ya Tanzania Gavana Mstaafu, Prof. Florens Luoga, mara baada ya mazungumzo yao yaliyofanyika tarehe 10 Aprili 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.

Gavana Mstaafu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, ameimwagia sifa Makumbusho ya Benki Kuu kwa kuwa na utajiri wa maudhui mbalimbali yanayoelezea historia ya fedha, historia ya Benki Kuu pamoja na mageuzi mbalimbali yaliyofanyika kwenye sekta ya fedha na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Prof. Luoga alitoa sifa hizo alipotembelea Makumbusho ya Benki Kuu ambapo alipokelewa na Naibu Gavana wa BoT, Dkt. Yamungu Kayandabila, katika ofisi za Makao Makuu ndogo ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam Aprili 10 2026.

"Hongereni sana kwa kuanzisha makumbusho hii kwa kuwa ni kitu chenye upekee. Upekee wake ni kwamba Benki Kuu hapa nchini ipo moja tu,kwa hiyo maudhui yake lazima yawe na upekee na yenye maana kubwa kwenye historia ya nchi.

Alieleza kuwa makumbusho hayo yatanufaisha makundi mbalimbali katika jamii, ikiwemo watafiti, wanafunzi wa ngazi tofauti za elimu pamoja na wananchi kwa ujumla kwa kuwapatia fursa ya kujifunza historia ya fedha nchini na kuelewa mchango wa Benki Kuu katika kusimamia na kustawisha uchumi wa taifa katika vipindi mbalimbali vya mabadiliko ya kiuchumi tangu kuanzishwa kwake Juni 14 1966.



Gavana Mstaafu, Prof Florens Luoga (kushoto), akielezea jambo alipotembelea Makumbusho ya Benki kuu Aprili 10 2026. Pamoja na yeye ni Naibu Gavana wa BoT, Dkt. Yamungu Kayandabila (katikati) na Afisa Uhusiano wa Umma , Bw. Daniel Mlimuka.




Afisa Uhusiano wa Umma wa BoT, Bw. Daniel Mlimuka, akitoa mukhtasari wa maudhui ya Makumbusho ya BoT kwa Gavana Mstaafu, Prof. Florens Luoga, aliyetembelea Makumbusho hiyo Aprili 10 2026.

Pia, Gavana huyo mstaafu aliipongeza Benki Kuu kwa kutengeza makumbusho hayo kwa kutumia wataalamu wa ndani ya taasisi akikitaja kitendo hicho kuwa ni cha kizalendo na kitapunguza utegemezi wa watoa huduma wa kigeni.

Katika hatua nyingine, Prof. Luoga alikutana na kufanya Mazungumzo na Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba.

Makumbusho ya Benki Kuu yalizinduliwa rasmi tarehe 30 Julai 2025 na Makamu wa Rais Mstaafu, Dkt. Philip Mpango. Makumbusho haya hufunguliwa siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kuanzia 3:00 Asubuhi hadi saa 9:00 Alasiri.




Gavana Mstaafu, Prof. Luoga (kushoto) katika mazungumzo na Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba (katikati) na Dkt. Yamungu Kayandabila (kulia) Aprili 10 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.

# SERIKALI: BOT ENDELEENI KULINDA WANANCHI DHIDI YA MIKOPO 'UMIZA'



Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Laurent Luswetula, akizungumza wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yaliyofanyika tarehe 21 Januari 2026 katika Viwanja vya Usagara mkoani Tanga.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeagizwa kuongeza juhudi za udhibiti wa sekta ya fedha kwa lengo la kuwalinda wananchi dhidi ya athari za kukopa katika taasisi zisizo rasmi.

Rai hiyo imetolewa na Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (MB), kupitia hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Laurent Deogratius Luswetula, wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yaliyofanyika Januari 21, 2026 katika Viwanja vya Usagara mkoani Tanga.

Waziri Omar alisema ukopaji katika taasisi zisizo rasmi husababisha wananchi wengi kupoteza mali na rasilimali zao za thamani kutokana na mikopo yenye masharti kandamizi.

Pia, amebainisha kuwa wananchi wengi wamekuwa wakipata athari mbalimbali kutokana na kukopa fedha katika taasisi zisizo rasmi, hivyo kusisitiza umuhimu wa wananchi kupata taarifa sahihi kuhusu uhalali wa taasisi za kifedha kabla ya kukopa.

"Kwa upande wa wananchi tunaomba msome na kujiridhisha mikataba ya mikopo mnayoingia ili kuepuka hasara zinazotokana na kusaini mikataba bila kuelewa masharti yake,"alisema Waziri Omar.

Kwa upande wake, Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, kupitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha wa BoT, Bw. Kennedy Komba, alisema kuwa katika kutekeleza sera za ujumuishi wa kifedha na kuongeza uwazi, ulinzi na ufikikaji wa huduma kwa watumiaji wa huduma za fedha, hususan kwa wale wenye malalamiko dhidi ya watoa huduma au wanaokosa taarifa kamili kuhusu gharama, tozo na utaratibu wa ukokotoaji wa riba na mikopo, BoT imeanzisha na kuimarisha mifumo mbalimbali.

"Mifumo hiyo ni pamoja na mifumo ya uwasilishaji na usimamizi wa malalamiko (SEMA na BOT), kilinganishi cha bei, kikokotoo cha gharama za mikopo, pamoja na utaratibu wa usimamizi shirikishi kwa watoa huduma ndogo za fedha wa kundi la pili, hatua ambazo zimeongeza uwazi, ufanisi na ubora wa huduma za fedha zinazotolewa kwa wananchi kwa kuzingatia matakwa ya sheria na kanuni zilizopo,"alisema Gavana Tutuba.

Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yalifanyika mkoani Tanga kuanzia Januari 19 hadi 26, 2026, yakiwa na lengo la kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya fedha na matumizi ya huduma rasmi za fedha kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.



Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Laurent Luswetula, akipewa maelezo kuhusu sarafu za ya ukumbusho na Meneja Idara ya Mawasiliano, Bi. Victoria Msina, alipotembelea banda la BoT katika Maonesho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa jijini Tanga.

## BOT YANYAKUA TUZO MBILI

Sambamba na maagizo hayo, pia wakati wa kufunga maonesho hayo BoT ilijinyakulia tuzo mbili pamoja na cheti cha ushiriki.

Katika maonesho hayo, BoT ilitoa elimu ya fedha kwa wananchi zaidi ya 3,000, hatua iliyoiwezesha kushinda Tuzo ya Uhamasishaji na Tuzo ya Udhamini, kama kutambua mchango wake mkubwa katika kuandaa na kufanikisha maonesho hayo.

Katika hotuba yake ya kufunga maonesho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dkt. Batlida Buriani aliwahimiza wananchi, hususan wanawake, kukopa katika taasisi za fedha zenye leseni ya Benki Kuu ya Tanzania ili kuepuka mikopo kandamizi kutoka kwa wakopeshaji wasio rasmi.




# WANAWAKE WATAJWA NGUZO YA MIFUMO JUMUISHI YA KIFEDHA

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania anayesimamia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, amesisitiza umuhimu wa kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi ili kufanikisha malengo ya ujumuishwaji wa kifedha nchini.

Bi. Msemo alisema hayo katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWIFA), wenye kaulimbiu isemayo: "Uongozi wa Wanawake kama Kichocheo cha Mifumo Jumuishi na Endelevu ya Kifedha: Kuendeleza NFIF III na FSDMP 2030" uliofanyika tarehe 23 Machi 2026 jijini Arusha.

Alieleza kuwa kufikiwa kwa malengo ya Mkakati wa Kitaifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha (NFIF III) na Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (FSDMP) kunahitaji jitihada za makusudi za kuziba pengo la kijinsia. Alisisitiza kuwa wanawake hawapaswi kuonekana tu kama wanufaika wa huduma za kifedha, bali washirikishwe kikamilifu kama wabunifu na wachangiaji wa mifumo bora ya kifedha.



Naibu Gavana, Bi. Sauda Msemo, akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWIFA) uliofanyika jijini Arusha tarehe 23 Machi 2026.




Alibainisha kuwa wanawake wengi wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa dhamana zinazokubalika na taasisi za fedha, kutokana na wengi wao kutomiliki mali zisizohamishika kama ardhi. Kutokana na hali hiyo, Benki Kuu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inaandaa rasimu ya sheria itakayoruhusu matumizi ya mali zinazohamishika ikiwemo vifaa, mazao, hisa na mali nyingine kama dhamana ya mikopo.

Aidha, Naibu Gavana alibainisha vikwazo vya kimasoko, ikiwemo uwepo wa bidhaa za kifedha zisizoendana na mahitaji ya wanawake, gharama kubwa za miamala na upatikanaji mdogo wa huduma katika maeneo ya vijijini. Alitoa wito kwa taasisi za fedha na kampuni za teknolojia ya fedha (Fintech) kuendelea kubuni bidhaa jumuishi zinazolenga kuwafikia wanawake, hususan waliopo katika sekta isiyo rasmi.

Kwa upande wa vikwazo vya watumiaji wa huduma, alitaja changamoto za uelewa mdogo wa masuala ya kifedha, mila na desturi, pamoja na uaminifu mdogo kwa taasisi rasmi za kifedha. Alisisitiza umuhimu wa kuimarisha elimu ya fedha na programu za kujenga uwezo, pamoja na kutumia mifumo ya kijamii kama vikundi vya kuweka akiba ili kuongeza ushiriki wa wanawake.

Mgeni rasmi katika mkutano huo alikuwa Mhe. Khamis Mussa Omar (Mb), Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Saada Mkuya Salum, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu – SMZ na Mlezi wa TAWIFA; Mwenyekiti wa TAWIFA, Fikiri Ntomola; Kamishna wa Bima Tanzania, Baghayo Abdallah Saqware; pamoja na Naibu Kamishna wa Bima, Hadija Said. Aidha, mkutano huo uliwakutanisha watendaji wakuu wa taasisi mbalimbali, maafisa waandamizi wa serikali na sekta binafsi, pamoja na washirika wa maendeleo.

# BOT YAPATA PIGO VIFO VYA MAGAVANA WASTAAFU WAWILI



Gavana Emmanuel Tutuba akizungumza na waombolezaji waliofika kwenye msiba wa hayati Dkt. Idris M. Rashid baada ya shughuli za mazishi zilizofanyika tarehe 14 Machi 2026 wilaya ya Mbulu mkoani Manyara.




Gavana Emmanuel Tutuba akiweka shada la maua katika kaburi la Hayati Edwin Isaac Mbiliewi Mtei, wakati wa shughuli za mazishi zilizofanyika jijini Arusha tarehe 24 Januari 2026. Kushoto ni Meneja Idara ya Mawasiliano, Bi. Victoria Msina.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imepata pigo kubwa kufuatia vifo vya magavana wawili wastaafu ndani ya kipindi cha miezi miwili, huku ikiahidi kuendelea kuenzi michango yao.

Mnamo Januari 19, 2026, Taifa lilimpoteza Gavana wa kwanza wa BoT, Hayati Edwin Isaac Mtei, aliyewahi kushika wadhifa huo kuanzia mwaka 1966 hadi 1974. Takribani miezi miwili baadaye, Machi 13, 2026, BoT ilimpoteza tena Gavana wa nne, Hayati Dkt. Idris M. Rashid, aliyewahi kuiongoza kuanzia mwaka 1993 hadi 1998.

Mazishi ya viongozi hao yalihudhuriwa na viongozi wa juu wa Serikali pamoja na wananchi, yakidhihirisha heshima kubwa waliyopewa kwa mchango wao katika maendeleo ya Taifa.

Katika mazishi ya Hayati Edwin Mtei yaliyofanyika jijini Arusha Januari 24, 2026, Gavana wa sasa wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, alieleza kuwa marehemu alikuwa nguzo muhimu katika kuanzishwa na kuimarishwa kwa Benki Kuu ya Tanzania. Alisisitiza kuwa njia bora ya kumuenzi ni kuendeleza misingi ya bidii, uwajibikaji na uadilifu aliyoiweka.

Aliongeza kuwa BoT itaendelea kusimamia uchumi wa taifa kwa kuweka sera thabiti na mifumo imara ya fedha ili kuhakikisha ukuaji endelevu wa uchumi.

Kwa upande wa Hayati Dkt. Idris M. Rashid, mazishi yake yalifanyika Machi 14, 2026 katika wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, ambapo Gavana Tutuba aliongoza mamia ya waombolezaji kutoa heshima za mwisho. Katika hotuba yake, alieleza kuwa Dkt. Rashid alitoa mchango mkubwa katika mageuzi ya kiuchumi nchini, hususan kupitia usimamizi wa mabadiliko ya Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995.

Alisema mageuzi hayo yaliweka msingi imara wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania, huku yakisaidia kuimarisha sekta ya fedha na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa sera za uchumi.
"Tunapaswa kumuenzi kwa kuendeleza uzalendo, uadilifu na bidii katika kazi, kwani hayo ndiyo maadili aliyoyaishi wakati wa utumishi wake," alisema Gavana Tutuba.

Aidha, alibainisha kuwa marehemu Dkt. Rashid alikuwa mtu mcha Mungu, mwenye upendo na moyo wa kusaidia wengine, akiwataka wananchi kuiga mienendo hiyo katika kujenga jamii yenye mshikamano na maelewano.

Mazishi hayo yalihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Mshamu Ali Munde (Mb), pamoja na wafanyakazi wa BoT na wananchi mbalimbali walioungana na familia kutoa heshima za mwisho.

Kwa ujumla, vifo vya viongozi hao wawili vinaacha pengo kubwa katika historia ya sekta ya fedha nchini. Hata hivyo, mchango wao unaendelea kuishi kupitia misingi waliyojenga, kuanzia uanzishwaji wa Benki Kuu hadi mageuzi ya kisera yaliyoweka dira ya uchumi wa Tanzania.

BoT imeeleza kuwa itaendelea kuenzi urithi huo kwa kuhakikisha taasisi inaendelea kusimamia kwa ufanisi uchumi wa Taifa, ikiwa ni sehemu ya kuendeleza maono ya viongozi hao waliolitumikia taifa kwa uadilifu na weledi mkubwa.



Gavana Emmanuel Tutuba pamoja na baadhi ya waombolezaji wakibeba jeneza la hayati Dkt. Idris M. Rashid katika shughuli za mazishi zilizofanyika tarehe 14 Machi 2026 wilaya ya Mbulu mkoani Manyara.

# BOT YAMWAGIWA SIFA USIMAMIZI THABITI SEKTA YA KIBENKI



Gavana, Bw. Emmanuel Tutuba, akiagana na Afisa Mtendaji Mkuu wa NCBA Group Kenya, Bw. John Gachora, baada ya kikao na viongozi wa NCBA Group Ltd. na Nedbank Group PLC. walipotembelea ofisi za BoT jijini Dar es Salaam. Kutoka kushoto ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Nedbank Group Ltd. Afrika ya Kusini, Bw. Jason Quinn, Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya NCBA Tanzania, Dkt. Fauz Twaib pamoja na Naibu Gavana wa BoT, Bi. Sauda Msemo.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imepongezwa kwa usimamizi wake thabiti wa sekta ya kibenki, hali inayochangia kuongezeka kwa faida za mabenki nchini pamoja na kukuza ustawi wa sekta ya fedha kwa ujumla.

Pongezi hizo zilitolewa na Afisa Mtendaji Mkuu wa NCBA Group Kenya, Bw. John Gachora, alipotembelea Benki Kuu Machi 30, 2026 na kufanya mazungumzo na Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba.

Mazungumzo hayo yalilenga kujadili dhamira ya Nedbank Group Limited kununua asilimia 66 ya hisa za NCBA Group PLC.

"Naipongeza BoT kwa usimamizi mzuri wa sekta ya kibenki. Ukiangalia takwimu, utagundua kuwa kuna ongezeko la faida kwa mabenki nchini kila mwaka. Hii inatokana na usimamizi madhubuti wa BoT pamoja na uwepo wa mazingira rafiki kwa mabenki kufanya shughuli zao," alisema.

Kwa upande wake, Gavana Tutuba aliikaribisha Nedbank Group Limited na wadau wengine kuwekeza nchini, akibainisha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri kiuchumi barani Afrika, hivyo kutoa fursa nyingi za uwekezaji.

"Kuwekeza Tanzania kunatoa fursa ya kufanya biashara katika soko pana, kutokana na uanachama wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), pamoja na makubaliano ya Eneo Huru la Biashara la Afrika," alisema.

Aidha, alisisitiza kuwa Benki Kuu itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuhakikisha mabenki yanaendelea kustawi. Pia alihimiza mabenki kutumia fursa ya upatikanaji wa umeme wa uhakika na kuimarika kwa teknolojia ya intaneti ili kubuni huduma za kidijitali zitakazoongeza ufanisi na kupanua upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Naibu Gavana wa BoT, Bi. Sauda Msemo, Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya NCBA Tanzania, Dkt. Fauz Twaib pamoja na Afisa Mtendaji Mkuu wa Nedbank Group Ltd. Afrika ya Kusini, Bw. Jason Quinn.

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2025, Tanzania ilikuwa na jumla ya benki 42 zilizosajiliwa. Kati ya hizo, 35 ni benki za biashara, tatu ni benki za huduma ndogo za fedha, mbili ni benki za jamii, na mbili ni benki za maendeleo.



Afisa Mtendaji Mkuu wa NCBA Group Kenya, Bw. John Gachora, akizungumza katika kikao na Gavana, Bw. Emmanuel Tutuba, kilichofanyika tarehe 30 Machi 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.



Afisa Mtendaji Mkuu wa Nedbank Group Ltd. Afrika ya Kusini, Bw. Jason Quinn, akizungumza katika kikao na Gavana, Bw. Emmanuel Tutuba, kilichofanyika tarehe 30 Machi 2026 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.



Gavana, Bw. Emmanuel Tutuba, akizungumza katika kikao na viongozi wa NCBA Group na Nedbank Group, walipotembelea BoT jijini Dar es Salaam kujadili kuhusu dhamira ya Nedbank Group Ltd. kununua asilimia 66 ya hisa za NCBA Group PLC.

# BOT YAPATA NAIBU GAVANA MPYA, MFAHAMU ZAIDI



Januari 29, 2026 Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iliamka na furaha kwa uteuzi wa Naibu Gavana mpya anayeshughulikia Utawala na Udhibiti wa Ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh.

Dkt. Rahma aliteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Saluhu Hassan kuchukua mikoba ya Bw. Julian Banzi Raphael aliyemaliza muda wake.

Akizungumza kwa mara ya kwanza na wafanyakazi wa BoT, katika hafla ya kumuaga Bw. Raphael iliyofanyika Februari 7, 2026 aliwasihi wafanyakazi kudumisha ushirikiano na mshikamano ili kuzidi kuimarisha utendaji wa shirika.

"Mimi ni mgeni katika familia hii ya Benki Kuu, lakini naamini uwepo wenu utawezesha kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Naomba ushirikiano mliompatia Bw. Raphael mnipatie na mimi," alisema Dkt. Rahma.

Awali kabla ya hafla hiyo, Dkt. Rahma aliwasili rasmi BoT Makao Makuu Ndogo Dar es Salaam Februari 3, 2026 na kupokelewa na Gavana Bw. Emmanuel Tutuba, pamoja na viongozi waandamizi.



Gavana Emmanuel Tutuba akiwa na Naibu Gavana, Dkt. Rahma Salim Mahfoudh, baada ya kumpokea katika Ofisi Ndogo ya Makao Makuu ya BoT jijini Dar es Salaam, tarehe 3 Februari 2026.

## NYADHIFA ALIZOWAHI KUSHIKA KABLA

Kabla ya uteuzi huo, Dkt. Rahma alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nafasi aliyodumu nayo kwa takribani miezi miwili baada ya kuteuliwa na Rais wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi.

Pia, aliwahi kuhudumu kama Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ya Zanzibar wakati anahudumu nafasi hiyo pia, alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Ukaguzi ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA).

Kwa uteuzi huu, Dkt. Rahma anakuwa mwanamke wa tatu katika historia ya BoT kushika nafasi ya Naibu Gavana. Uteuzi wake unafuatia ule wa Sauda Msemo ambaye aliteuliwa na Rais Samia tarehe Juni 1, 2022 kuwa Naibu Gavana anayesimamia Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha.

Mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo alikuwa Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, ambaye kwa sasa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, aliyeteuliwa mwaka 2011.

# NAIBU GAVANA RAPHAEL ASTAAFU, BOT YAMUAGA



Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, akimkabidhi Zawadi ya ukumbusho Naibu Gavana, Bw. Julian Raphael, katika hafla maalumu ya kumuaga mstaafu huyo iliyofanyika tarehe 06 Machi, 2026.

> *Kwa kweli mmenishangaza, sikutegemea upendo huu. Nawashukuru sana. Kwa Naibu Gavana aliyepokea kijiti changu, namhakikishia asiwe na wasiwasi kwa kuwa Benki Kuu ina wataalamu wazuri watakaomshauri ipasavyo.*
>
> *Bw. Julian Raphael*

Miaka 10 ya weledi na utumishi uliotukuka katika kuitumikia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilitimia Februari 2026 kwa aliyekuwa Naibu Gavana Utawala na Udhibiti wa Ndani, Bw. Julian Banzi Raphael.

Hiyo ikafanya tamati ya utumishi wake ndani ya BoT aliouanza mwaka 2016 kwa kufanyiwa hafla maalum ya kumuaga na kumtakia heri katika maisha yake nje ya Benki.

Hafla hiyo ilifanyika Februari 6, 2026 katika Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam, ikilenga kutambua na kuthamini mchango wake.



Akizungumza katika hafla hiyo, Gavana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, alimpongeza Bw. Raphael kwa utumishi wake uliotukuka uliojaa uadilifu, kujituma na uzalendo.

"Natumia fursa hii kumpongeza Mzee Julian Raphael kwa kuitumikia Benki Kuu kwa miaka 10. Ni jambo kubwa sana, hususan unapomaliza salama. Kwa watumishi tuliopo tunasema Mzee Raphael hatukudai," alisema Gavana Tutuba.

Aliongeza kuwa Bw. Raphael aliiongoza BoT kwa uadilifu, alitoa miongozo muhimu na alijikita katika kuwalea na kuwajenga watumishi vijana, huku akitambua umuhimu wa kusaidia watu katika utekelezaji wa majukumu yake.

Pia, katika hafla hiyo Gavana Tutuba alimkaribisha Naibu Gavana mpya wa BoT, Dkt. Rahma Mahfoudh, aliyeteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 25 Januari 2026 na kuanza kazi rasmi Februari 3, 2026.


"Tunakukaribisha Dkt. Rahma Mahfoudh katika familia ya Benki Kuu ya Tanzania. Tunakuahidi ushirikiano kutoka kwa wafanyakazi wote, na hatuna shaka kuwa utaweza kuvivaa viatu vya mstaafu Bw. Raphael," alisema Gavana Tutuba.

Kwa upande wake, Naibu Gavana mstaafu, Bw. Julian Raphael, aliwashukuru wafanyakazi wa Benki Kuu kwa ushirikiano mkubwa waliompatia katika kipindi chote cha utumishi wake, akieleza kufarijika na upendo waliouonesha.



Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, katika picha ya pamoja na Naubu Gavana Mstaafu, Bw. Julian Raphael pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Benki Kuu baada ya kutamatika kwa hafla ya kumuaga Naibu Gavana huyo.

# BOT YASHIRIKISHA WADAU MPANGO WA KUANZISHA KAMPUNI YA UDHAMINI WA MIKOPO




Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila pamoja na wadau baada ya kikao kilichofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 12 Machi 2026.



Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, akielezea jambo katika kikao na wadau kilichofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 12 Machi 2026.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ikiongozwa na Naibu Gavana wa Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, ilifanya kikao na wadau mbalimbali kujadiliana kuhusu mpango wa kuanzishwa kwa kampuni ya utoaji na usimamizi wa dhamana za mikopo itakayojulikana kama Tanzania Credit Guarantee PLC.

Kikao hicho kilichofanyika, tarehe 12 Machi 2026, katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam, kimewakutanisha wadau kutoka taasisi mbalimbali ikiwemo Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Kampuni za Bima, Mifuko ya Pamoja ya Uwekezaji wa Mitaji, Mifuko ya Pensheni pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

Mpango wa kuanzishwa kwa kampuni hiyo unalenga kuendana na ukubwa na kasi ya utekelezaji unaohitajika kufanikisha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ambayo inalenga kuimarisha uchumi wa Tanzania na kuongeza mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya taifa.

Vilevile, kampuni hiyo itasaidia kutenganisha majukumu ya Benki Kuu ya udhibiti na utoaji wa dhamana za mikopo, hivyo kuondoa mgongano wa maslahi na kuboresha ufanisi wa kiutendaji. Pia itahamasisha ubunifu pamoja na kuongeza uwezo wa taasisi husika kujibu kwa haraka mahitaji ya soko.

Kwa sasa, Benki Kuu ya Tanzania inasimamia mifuko miwili ya udhamini wa mikopo ambayo ni Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo ya Nje (Export Credit Guarantee Scheme – ECGS) na Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SME Credit Guarantee Scheme – SME-CGS).

Serikali ilianzisha mifuko hiyo kwa lengo la kudhamini benki na taasisi za fedha ili kuimarisha utoaji wa mikopo kwa wakopaji wenye miradi yenye tija lakini wanaokabiliwa na upungufu wa dhamana. Lengo kuu ni kuwezesha mazingira rafiki ya kukuza na kuendeleza miradi ya maendeleo, kuongeza ajira, kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni kupitia mauzo ya nje na kuchangia ukuaji wa pato la Taifa.



Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), CPA Nicodemus Mkama, akichangia mada katika kikao na wadau kilichofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 12 Machi 2026.



Kamishna wa Bima Tanzania, Dr. Baghayo Abdallah Saqware, akichangia mada katika kikao na wadau kilichofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 12 Machi 2026.

# KAMATI YA BAJETI YAIPONGEZA BOT KUSIMAMIA UCHUMI, YATOA MAELEKEZO

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeipongeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kutekeleza majukumu yake huku ikiipa maelekezo ya maeneo ya kutilia mkazo zaidi ili kusimamia vyema uthabiti wa sekta ya fedha.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye pia ni Mbunge wa Maswa Magharibi, Mhe. Mashimba Ndaki, Februari 10, 2026 ambaye alisema;

"Niwapongeze Benki Kuu kwa kusimamia vyema majukumu yenu, hili linaonekana waziwazi kwa namna Gavana Tutuba alivyokuwa anajibu maswali ya wajumbe wa kamati. Unaona kabisa kuwa huyu mtu anaifahamu vizuri taasisi yake.

"Jambo la muhimu, pale waheshimiwa wabunge walipowashauri mpawekee mkazo ili mfanye vizuri zaidi hususani katika riba za mikopo ya benki za biashara na kusimamia vyema udhamini wa mikopo wa wajasiriamali," alisema na kuongeza Mhe. Ndaki.

Mhe. Ndaki aliongeza kuwa wanaipongeza BoT kwa hatua ilizochukua kukabiliana na changamoto ya uhaba wa dola za Marekani iliyokuwepo awali, hali iliyosaidia kurejesha utulivu katika soko la fedha za kigeni.

Kwa upande wa ujumbe wa BoT Gavana Bw. Emmanuel Tutuba, ambaye alitoa wasilisho kuhusu muundo, majukumu na utekelezaji wa kazi za Benki Kuu kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Wasilisho hilo pia lilihusisha majibu ya hoja na maswali mbalimbali yaliyoulizwa na wajumbe wa kamati hiyo.

Lengo la wasilisho hilo lilikuwa ni kuwajengea uelewa wajumbe wa Kamati ya Bajeti kuhusu namna Benki Kuu inavyotekeleza majukumu yake ya msingi, ikiwemo usimamizi wa sera ya fedha, akiba ya taifa pamoja na udhibiti wa watoa huduma katika sekta ya fedha.

Akitoa wasilisho hilo, Gavana Tutuba alisema BoT imelenga kuboresha jukumu lake la udhamini wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kufungua kampuni itakayosimamia suala hilo.

"Kwa kutambua kuwa jukumu hili ni nyeti katika uchechemuzi wa uchumi, tupo mbioni kufungua kampuni ya udhamini wa mikopo ili kuwafikia watu wengi zaidi na huko mbeleni tuna mkakati kila benki ya biashara iwe na dirisha ambalo hata mhitimu aliyemaliza kada ya kilimo apelike cheti chake na akubaliwe kupewa mkopo wa mradi aliouandaa," alisema Gavana Tutuba.

Kikao hicho kimefanyika ikiwa ni siku 28 tangu kamati za kudumu za Bunge ziundwe na kuchagua viongozi wake.



Baadhi ya wakurugenzi na mameneja wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) wakifuatilia wasilisho la Gavana Tutuba kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba akitoa wasilisho kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.



Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Ally Hassan Omar King akitoa hoja baada ya wasilisho lililotolewa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania.

# GAVANA TUTUBA AANGAZIA NGUVU YA TEKNOLOJIA YA FEDHA



Gavana Emmanuel Tutuba, akifafanua jambo katika moja ya mijadala ya Kikao cha 58 cha Tume ya Uchumi ya Afrika (ECA), kilichofanyika jijini Tangier, Morocco, kuanzia tarehe 2 Aprili 2026.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, amesema kuwa teknolojia ya fedha inamchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi, akieleza kuwa inaongeza kasi ya miamala, inapunguza gharama za huduma na kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa watu wengi zaidi, wakiwemo walioko maeneo ya mbali.

Gavana Tutuba aliyasema hayo alipokuwa akichangia katika mjadala wa mawaziri wakati wa Kikao cha 58 cha Tume ya Uchumi ya Afrika (ECA), kilichofanyika jijini Tangier, Morocco, kuanzia tarehe 28 Machi hadi 3 Aprili 2026. Kikao hicho kiliwakutanisha Mawaziri wa Fedha, Mipango na Maendeleo ya Uchumi pamoja na Magavana wa Benki Kuu kutoka nchi mbalimbali za Afrika, kujadili mwelekeo wa uchumi wa bara hilo.

Katika mchango wake, Gavana Tutuba alibainisha kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika ujumuishaji wa kifedha kupitia huduma za fedha kwa njia ya simu na mifumo ya malipo yakidigitali yenye ufanisi. Amesema mafanikio hayo yamechangia kupunguza gharama za miamala, kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya serikali na kuongeza uwazi katika matumizi ya fedha.




Gavana Emmanuel Tutuba akijadiliana jambo na Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), wakati wa Kikao cha 58 cha Tume ya Uchumi ya Afrika (ECA), kilichofanyika jijini Tangier, Morocco, kuanzia tarehe 28 Machi hadi 3 Aprili 2026.

Aidha, alieleza kuwa Tanzania ni sehemu ya mifumo ya malipo ya kikanda ikiwemo Mfumo wa Malipo wa Afrika Mashariki (EAPS) na Mfumo wa Malipo wa Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SADC RTGS). Vilevile, alibainisha kuwa benki za biashara nchini zinaendelea kujiunga na Mfumo wa Malipo wa Afrika (PAPSS), unaowezesha miamala ya kifedha kati ya nchi za Afrika kwa haraka na ufanisi, hatua itakayochochea biashara na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi barani Afrika.

Akizungumzia Dira ya Taifa ya Maendeleo kuelekea mwaka 2050, Gavana Tutuba amesisitiza kuwa teknolojia ya fedha pamoja na teknolojia nyingine za kidijitali zitaendelea kuwa nguzo muhimu katika kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani.

Katika kukuza ubunifu, Gavana alieleza kuwa Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa vijana wabunifu kupitia majukwaa mbalimbali ya ubunifu ili kuibua suluhisho za kidijitali zitakazoboresha huduma za kifedha.

Vilevile, amesema Benki Kuu inaendelea kutumia akili unde (AI) na imesaini makubaliano na vyuo vikuu mbalimbali nchini kwa lengo la kuendeleza tafiti zitakazosaidia matumizi mapana ya teknolojia hiyo katika sekta ya fedha.



Gavana Emmanuel Tutuba katika moja ya mijadala ya Kikao cha 58 cha Tume ya Uchumi ya Afrika (ECA), kilichofanyika jijini Tangier, Morocco, kuanzia tarehe 2 Aprili 2026.

# BOT YASISITIZA USHIRIKIANO WA KIKANDA KUIMARISHA MIFUMO YA MALIPO




Naibu Gavana, Bi. Sauda Kassim Msemo, akizungumza jambo wakati wa kufunga kikao cha pamoja cha usimamizi wa mifumo ya malipo na ulipaji kwa nchi za Afrika Mashariki kilichofanyika katika ukumbi wa Benki Kuu jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 30 Machi hadi 2 Aprili 2026.

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bi. Sauda Kassim Msemo, amesisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kikanda katika kuimarisha usimamizi wa mifumo ya malipo na ulipaji, akieleza kuwa katika mazingira ya sasa ya kidijitali, hakuna benki kuu inayoweza kufanya kazi kwa ufanisi ikiwa peke yake.

Bi. Msemo alitoa kauli hiyo wakati wa kufunga kikao cha pamoja cha usimamizi wa mifumo ya malipo na ulipaji kwa nchi za Afrika Mashariki kilichofanyika katika ukumbi wa Benki Kuu jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 30 Machi hadi 2 Aprili 2026.

Alieleza kuwa kwa muda wa siku nne, kikao hicho kimewakutanisha wataalamu mbalimbali waliokuwa na lengo la pamoja la kuimarisha uwazi, uthabiti na ufanisi wa mifumo ya malipo na ulipaji.

Alipongeza kiwango cha ushiriki, uwazi wa mijadala pamoja na kubadilishana uzoefu wa vitendo miongoni mwa washiriki, akibainisha kuwa yote hayo yamewajengea uwezo zaidi katika kutekeleza majukumu yao.

"Ujumbe mmoja muhimu umejitokeza katika majadiliano yetu—katika dunia ya sasa ya mifumo ya fedha ya kidijitali inayokua kwa kasi, ushirikiano wa kikanda si hiari, bali ni lazima," alisema.



Naibu Gavana, Bi. Sauda Kassim Msemo, akifunga kikao cha pamoja cha usimamizi wa mifumo ya malipo na ulipaji kwa nchi za Afrika Mashariki kilichofanyika katika ukumbi wa Benki Kuu jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 30 Machi hadi 2 Aprili 2026.

Aidha, alisisitiza kuwa kuongezeka kwa muingiliano wa mifumo ya malipo kunahitaji mbinu za pamoja, thabiti na za mbele katika usimamizi, hasa katika maeneo ya usimamizi unaozingatia vihatarishi, uzingatiaji wa kanuni za kupambana na utakatishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi (AML/CFT/CPF), ufuatiliaji wa miamala na utawala bora.

Akizungumzia ziara ya washiriki katika huduma ya kifedha ya kidijitali ya Mixx by Yas, Bi. Msemo alisema imewapatia washiriki uelewa wa vitendo kuhusu fursa na changamoto za ubunifu wa teknolojia ya kifedha (fintech), na kusisitiza kuwa usimamizi madhubuti unapaswa kuzingatia si tu sera bali pia uhalisia wa kiutendaji wa taasisi zinazosimamiwa.

Bi. Msemo alihitimisha kwa kueleza kuwa Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kujenga na kuimarisha miundombinu ya masoko ya fedha, kuboresha mifumo ya udhibiti na usimamizi, pamoja na kushirikiana kwa karibu na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sekretarieti ya EAC katika kufanikisha malengo ya pamoja.




Mkurugenzi wa Mifumo ya Malipo ya Taifa, Bi. Lucy Shaidi, akizungumza jambo wakati wa kufunga kikao cha pamoja cha usimamizi wa mifumo ya malipo na ulipaji kwa nchi za Afrika Mashariki kilichofanyika katika ukumbi wa Benki Kuu jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 30 Machi hadi 2 Aprili 2026.

# BOT: MIFUMO YA MALIPO NI MSINGI WA UKUAJI WA UCHUMI JUMUISHI



Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, akifafanua jambo kwa wanafunzi wa Shahada ya Uzamili ya Biashara (MBA) kutoka Chuo Kikuu cha Stanford, Marekani, walipotembelea Benki Kuu ya Tanzania jijini Dar es Salaam kujifunza kuhusu Mifumo ya Malipo ya Taifa inayosimamiwa na BoT.

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) anayeshughulikia Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, amesema kuwa mifumo ya malipo ya Taifa ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi jumuishi na kuimarisha ujumuishwaji wa kifedha nchini.

Akitoa hotuba ya ukaribisho kwa wanafunzi wa Shahada ya Uzamili ya Biashara (MBA) kutoka Chuo Kikuu cha Stanford, Marekani, waliotembelea BoT jijini Dar es Salaam Machi 28 2026, Dkt. Kayandabila alieleza kuwa mifumo ya malipo inachangia ukuaji wa uchumi shirikishi kwa kuwezesha malipo ambayo yanachochea ugavi katika uchumi na kuwa uti wa mgongo wa Uthabiti wa Sekta ya Fedha.

Alibainisha kuwa mifumo ya malipo yenye ufanisi, iliyo salama na shirikishi huchochea ufanisi wa sera ya fedha kwa kuwezesha uenezaji mzuri wa mabadiliko ya viwango vya riba vya Benki Kuu na kuimarisha udhibiti wa ukwasi ndani ya uchumi.

Dkt. Kayandabila alisema Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisera na kuwekeza katika miundombinu ili kuimarisha na kuboresha mifumo ya malipo, sambamba na kuchochea ubunifu hususan katika huduma za kifedha za kidijitali na ujumuishwaji wa kifedha.

Akifafanua kuhusu historia ya maboresho hayo, alisema kuwa mchakato wa kisasa wa mifumo ya malipo ulianza katikati ya miaka ya 1990 kama sehemu ya mageuzi mapana ya sekta ya fedha yaliyolenga kuongeza ufanisi, usalama na uthabiti wa mfumo wa fedha.

Aliongeza kuwa mageuzi hayo yaliwezesha kuingia kwa benki binafsi za ndani na za kimataifa, ubinafsishaji wa baadhi ya benki za serikali pamoja na kuondolewa kwa baadhi ya vikwazo katika huduma na bidhaa za kifedha.

Kwa mujibu wa Dkt. Kayandabila, mwaka 1996 BoT ilianzisha Mradi wa Maboresho ya Mifumo ya Malipo ya Taifa uliolenga kubadilisha mfumo wa zamani uliotegemea zaidi fedha taslimu na karatasi kuwa mfumo wa kielektroniki unaoendana na viwango vya kimataifa.

Alikumbusha kuwa kabla ya maboresho hayo, matumizi ya fedha taslimu yalitawala, huku hundi zikichukua hadi siku 14 kukamilisha miamala mikoani na siku 7 jijini Dar es Salaam, hali iliyokuwa ikichelewesha shughuli za kiuchumi.

Aidha, alisisitiza kuwa BoT inaendelea kufuatilia maendeleo ya teknolojia za mifumo ya malipo duniani na kushirikiana na wadau wa kikanda na kimataifa ili kunufaika na ubunifu huo, huku ikiendelea kulinda uthabiti wa sekta ya fedha, uadilifu wa mifumo na maslahi ya watumiaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mifumo ya Malipo ya Taifa, Bi. Lucy Shaidi, akielezea hatua muhimu zilizofikiwa katika safari ya kuendeleza mifumo ya malipo hadi kufikia mwaka 2025, alisema kuwa kumekuwapo na ukuaji wa kasi wa malipo ya papo kwa papo, huduma za fedha kupitia simu za mkononi, pamoja na mifumo ya malipo inayoweza kuunganishwa. Alibainisha kuwa maendeleo hayo yanaendelea kuichochea Tanzania kuelekea katika mfumo wa fedha uliojumuishi zaidi, wenye ufanisi, na unaotegemea kwa kiasi kikubwa teknolojia za kidijitali.

Miongoni na mafanikio makubwa ya Benki Kuu katika mifumo ya malipo ni kuanzishwa kwa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Hapo (Tanzania Instant Payment System – TIPS) unaoruhusu watumiaji wa huduma za fedha kutuma na kupokea fedha papo hapo , bila kujali taasisi ya kifedha wanayotumia. TIPS umeongeza ufanisi, umepunguza gharama za miamala, na kuimarisha ujumuishwaji wa kifedha kwa kurahisisha miamala ya kifedha kwa watu binafsi na biashara nchini Tanzania.



Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila pamoja na wanafunzi wa Shahada ya Uzamili ya Biashara (MBA) kutoka Chuo Kikuu cha Stanford, Marekani, walipotembelea Benki Kuu ya Tanzania jijini Dar es Salaam kujifunza kuhusu Mifumo ya Malipo ya Taifa inayosimamiwa na BoT.



Mkurugenzi wa Mifumo ya Malipo ya Taifa, Bi. Lucy Shaidi, akimkabidhi zawadi ya ramani ya Tanzania Profesa Zhiguo He kutoka Chuo Kikuu cha Stanford Marekani.

# WATAALAMU BENKI KUU EAC WAKUNA VICHWA KUONGEZA UJUMUISHAJI HUDUMA ZA KIFEDHA




Naibu Gavana, Bi. Sauda Kassim Msemo, akizungumza wakati wa ufunguzi wa warsha iliyofanyika tarehe 28 hadi 30 Januari 2026 katika Tawi la Benki Kuu ya Tanzania, Arusha.

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bi. Sauda Msemo, amesema kuwa ujumuishaji wa huduma za fedha na kuwalinda watumiaji wake ni nguzo muhimu katika kuimarisha sekta za fedha na kufikia maendeleo jumuishi na endelevu kwa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Bi. Msemo ameyasema hayo wakati wa ufunguzi wa warsha iliyofanyika Januari 28 -30, 2026 katika Tawi la Benki Kuu ya Tanzania, Arusha, ukiwakutanisha wajumbe kutoka Benki Kuu za nchi za Afrika Mashariki.

Alisisitiza kuwa mkutano huo ni jukwaa muhimu la kujadili na kuratibu mikakati ya pamoja ya kuongeza upatikanaji na matumizi ya huduma jumuishi za fedha pamoja na kuwalinda watumiaji wa huduma hizo, hatua itakayosaidia kupunguza umaskini na kuongeza ustawi wa wananchi wa ukanda huo.


"Washiriki wa mkutano huu mnapaswa kujikita katika kutatua changamoto zinazokwamisha matumizi ya huduma rasmi za fedha, hususan kwa makundi ya wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na wafanyabiashara wadogo. Makundi haya ni muhimu katika kufikia maendeleo jumuishi na endelevu,"alisema Naibu Gavana Sauda.

Akizungumza awali, Mkurugenzi wa Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha wa BoT, Bw. Kennedy Komba, alisema kuwa kupitia kamati hiyo, nchi wanachama zitaweza kuunda sera bora kwa kutumia taarifa zilizoratibiwa, mifumo ya vipimo na kazi ya uchambuzi wa pamoja.

huku wakihakikisha kuwa ustawi wa watumiaji, ustahimilivu wa kifedha na ukuaji jumuishi vinaendelea kuwa nguzo kuu za ajenda ya ujumuishaji wa sekta ya fedha katika Afrika Mashariki.

Aidha, alisema kuwa majadiliano ya kitaalamu katika mkutano huo yanajikita katika maeneo muhimu yakiwemo huduma jumuishi za fedha, viwango vya taarifa, mfumo wa vipimo vya afya ya kifedha (financial health) na ulinzi wa watumiaji wa huduma za fedha.

Majadiliano hayo yalilenga kuonesha umuhimu wa kuanzishwa kwa Kamati ya Wataalamu wa Huduma Jumuishi za Fedha na Ulinzi wa Watumiaji wa Huduma za Fedha, itakayosaidia kushughulikia masuala ya mshikamano wa kiuchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika eneo la ujumuishaji wa



Naibu Gavana, Bi. Sauda Kassim Msemo (katikati) pamoja na washiriki wa warsha iliyofanyika tarehe 28 hadi 30 Januari 2026 katika Tawi la Benki Kuu ya Tanzania, Arusha.

# WAZIRI WA FEDHA SMZ ATEMBELEA BOT ZANZIBAR, ATOA MAAGIZO



Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dkt. Juma Akil (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi wa Tawi la BoT Zanzibar, Bw. Ibrahim Malogoi, alipotembelea ofisi hizo Januari 14, 2026.

Wakati uchumi wa Zanzibar ukiendelea kukua kwa kasi, Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Dkt. Juma Akili amesema matumizi ya mifumo ya kidijiti katika sekta ya fedha ni jambo muhimu na la kuzingatiwa.

Dkt. Akili ameyasema hayo Januari 14, 2026 alipotembelea Makao Makuu Ndogo ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Zanzibar.

Mbali na masuala ya mifumo ya kidijiti, pia alitembea ofisi hizo kwa ajili ya kujadiliana masuala kimkakati yanayohusu usimamizi wa fedha na maendeleo ya uchumi wa Zanzibar.

"Bado naendelea kusisitiza tuimarishe zaidi matumizi ya mifumo ya ya kidijiti katika malipo ili kusimamia na ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha mapato hayo yanakusanywa kwa ufanisi na kwa usahihi,"

Aliongeza kuwa matumizi ya teknolojia ya kidijiti yana mchango mkubwa katika kuimarisha uwazi, uwajibikaji na usimamizi bora wa fedha za umma.

Pia, Dkt. Akili alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana kwa karibu na Benki Kuu ya Tanzania katika kuhakikisha uthabiti wa sekta ya fedha na kukuza uchumi jumuishi unaowanufaisha wananchi.

Aidha, Dkt. Akili alielekeza kuendelezwa kwa miradi ya maendeleo ya kimkakati kwa kuzingatia matumizi bora ya mapato ya ndani, akisisitiza kuwa mifumo ya kidijiti husaidia kupunguza utegemezi wa mikopo na kuimarisha maendeleo endelevu ya uchumi wa Zanzibar.

Ziara hiyo ni ya kwanza kwa waziri huyo tangu kuteuliwa kwake kushika wadhifa huo mwaka 2025 visiwani Zanzibar.

## HALI YA UKUAJI WA UCHUMI ZANZIBAR

*Wakati Dkt. Akili akitoa maelekezo hayo, ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2026 unatarajiwa kuwa **asilimia 6.8**, huku katika robo ya kwanza ya mwaka 2026 unatarajiwa kukua kwa **asilimia 7.2**.*




# BOT MWENYEJI MKUTANO WA BODI YA UTHABITI WA SEKTA YA FEDHA

Benki Kuu ya Tanzania iliandaa mkutano wa Bodi ya Uthabiti wa Sekta ya Fedha (Financial Stability Board-FSB) uliofanyika katika Hoteli ya the Mora, Zanzibar tarehe 20 Februari 2026 ukiwahusisha Magavana, Manaibu Gavana na maofisa waandaamizi kutoka Benki Kuu za kusini mwa Jangwa la Sahara.

FSB ni chombo cha kimataifa ambacho hufuatilia na kutoa mapendekezo kuhusu mfumo wa fedha duniani kwa lengo la kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha kwa kuandaa miongozo ya kuzisaidia nchi wanachama kuboresha sekta hiyo.

Akizungumza wakati anafungua mkutano huo, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, alisema mkutano wa FSB unatoa fursa kwa benki kuu wanachama kujadili namna ya kudhibiti athari mbalimbali zinazoweza kusababisha sekta ya fedha ikafanya vibaya.

"Miongoni mwa masuala yatakayojadiliwa katika mkutano huu ni pamoja na: Tathmini ya mwenendo wa viashiria vya uthabiti wa sekta kidunia na kikanda, athari za uthabiti wa sekta ya fedha unaotokana na na uhimilivu wa madeni, masuala ya Kifedha yasiyo ya Kibenki (NBFI) na Matumizi ya Teknolojia ya Akili Unde katika kuboresha utendaji wa sekta ya fedha pamoja na athari zake". Alisema Gavana Tutuba.

Aidha, alisisitiza kuwa ushiriki wa BoT katika mkutano huu unadhihirisha kuwa Benki Kuu inasimamia sekta ya fedha kwa mifumo inayokubalika kimataifa.

"Kupitia mkutano huu wananchi wanatakiwa kufahamu kuwa sisi BoT tunaendelea kusimamia sekta ya fedha kwa misingi na mifumo inayokubalika kimataifa na kwamba popote wanapohifadhi fedha zao watambue zipo salama na zinaendelea kutunzwa katika mifumo inayoendana na sheria na taratibu za kimataifa". Alieleza

Miongoni mwa mafanikio ambayo BoT imeyapata kwa kuwa mwananchama wa FSB ni pamoja na kuanzishwa kwa muundo wa kutambua idadi ya benki muhimu,njia za kutathmini mwingiliano wa mifumo ya kifedha, tathmini ya majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi, muundo wa unyumbulifu wa kukabiliana na dharura, miongozo ya kujiandaa na majanga ya kifedha na miundo mingine ya kusimamia sarafu mtandao na vihatarishi vya taasisi za kifedha zisizokuwa za kibenki.



Gavana Emmanuel Tutuba, akizungumza katika mkutano wa Bodi ya Uthabiti wa Sekta ya Fedha uliofanyika tarehe 20 Februari 2026, Zanzibar.



Naibu Gavana wa BoT (uthabiti na usimamizi wa sekta ya fedha), Bi. Sauda Msemo, akizungumza katika mkutano wa Bodi ya Uthabiti wa Sekta ya Fedha uliofanyika tarehe 20 Februari 2026, Zanzibar.




Manaibu Gavana wa BoT, Bi. Sauda Msemo (kushoto) na Dkt. Rahma Mahfoudh (kulia) pamoja na Naibu Kamishna wa Bima, Bi. Khadija Said (katikati), katika Mkutano wa FSB tarehe 20 Februari 2026 Zanzibar.



# BOT, CIC ZAJADILI FURSA ZA UWEKEZAJI

Ujumbe wa CIC ulioongozwa na Afisa Mkuu wa Usimamizi wa Vihatarishi na Makamu wa Rais Mtendaji, Bw. Guo Xiangjun, katika kikao na Gavana Emmanuel Tutuba, kilichofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 24 Machi 2026.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, alifanya kikao na ujumbe kutoka Shirika la Uwekezaji la China (China Investment Corporation – CIC) ulioongozwa na Afisa Mkuu wa Usimamizi wa Vihatarishi na Makamu wa Rais Mtendaji, Bw. Guo Xiangjun. Kikao hicho kimefanyika kwa njia ya mtandao tarehe 24 Machi 2026.

Katika kikao hicho, Gavana Tutuba alieleza kuwa Serikali ya Tanzania imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kuweka sera na mifumo rafiki pamoja na kupunguza urasimu, hatua inayolenga kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Aidha, alibainisha kuwa kwa sasa Serikali inatekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inayolenga kuifikisha Tanzania katika hadhi ya nchi yenye uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu. Katika utekelezaji wa dira hiyo, matarajio ni kwamba ifikapo mwaka 2050, pato la taifa litafikia thamani ya dola za Marekani trilioni moja, huku wastani wa pato la mtu mmoja ukifikia dola za Marekani 7,000 kwa mwaka.

Katika kufanikisha azma hiyo, Gavana Tutuba alizitaja sekta mbalimbali zenye fursa kubwa za uwekezaji, ikiwemo kilimo, utalii, viwanda na uzalishaji, madini, uchumi wa buluu, michezo na ubunifu, sekta ya fedha pamoja na sekta ya huduma.


Mwisho wa kikao hicho, pande zote mbili ziliazimia kuendeleza na kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya uwekezaji, kubadilishana uzoefu pamoja na kujenga uwezo, kwa lengo la kukuza maendeleo ya sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla.





Gavana Emmanuel Tutuba akiongoza kikao na ujumbe wa CIC kilichofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 24 Machi 2026.

# KIBONZO



Shoga yangu kuna mchezo unaanza wiki ijayo, unatoa elfu 2 kwa siku, kila baada ya siku 5 anatoka mtu 1 kwa laki 2. Tuchukue majina mawili mawili udugu wangu.
Ah! usijichanganye shoga yangu. Wiki iliyopita kuna mchezo kama huo uliharibika. Nilikuwa nachangia elfu 5 kila siku, lakini ilipofika zamu yangu kupokea, nikaambiwa fedha zimeibiwa.
Ni bora tuweke fedha zetu kwenye VICOBA vilivyosajiliwa na vinavyotambulika kisheria, ili ziwe salama na tuepuke hasara.
60TH ANNIVERSARY 1966 – 2026

# BOT YAPIGA MARUFUKU FEDHA KUTUMIKA KAMA SHADA LA MAUA



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba akizungumza katika mahojiano maalumu na Mhariri Mkuu wa Crown Media, Salim Kikeke, Makao Makuu ya BoT jijini Dodoma.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, amewaonya wananchi wanaozifunga fedha kama shada la maua kwa ajili ya zawadi kwa wapendwa wao, hususan katika kipindi cha msimu wa Sikukuu ya Wapendanao (Valentine) na mahafali.

Akizungumza katika mahojiano maalumu yaliyofanyika Alhamisi, Februari 12, 2026, ofisini kwake jijini Dodoma, Gavana Tutuba alisema kitendo hicho ni ukiukwaji wa sheria na husababisha uharibifu wa fedha hivyo wananchi waache.

Alisema kuwa fedha ni tunu ya Taifa, na utaratibu wa kuziweka katika mashada ya maua mara nyingi huhusisha kubandikwa kwa gundi pamoja na kukunjwa, hali inayochangia kuchakaa kwa haraka au kuchanika.

Kutokana na uharibifu huo, Benki Kuu hulazimika kuchapisha fedha mpya mara kwa mara, jambo linaloongeza gharama kwa Taifa.

"Hizi fedha tunazichapisha kwa gharama kubwa. Zinapobandikwa gundi na kukunjwa hovyo zinachakaa mapema, hivyo BoT inalazimika kuchapisha fedha mara kwa mara. Kama unataka kumpa zawadi ya Valentine mpendwa wako, mnunulie bidhaa yenye thamani au mpatie fedha hizo zikiwa katika hali yake ya kawaida," alisema Gavana Tutuba.

Aidha, Gavana Tutuba alisisitiza kuwa kila anayeshika fedha ya Tanzania ana wajibu wa kuzitunza na kuzihifadhi, kwa kuwa ni miongoni mwa alama na tunu muhimu za Taifa.


Gavana Tutuba alisema adhabu ya mtu anayekutwa na hatia ya kufanya hivyo au kuziharibu fedha ni faini ambayo inafika hadi TZS 5 milioni, japokuwa Benki Kuu kwa sasa imejikita zaidi kutoa elimu kwa jamii kuhusu suala hilo.

Katika hatua nyingine, kuhusiana na elimu ya utunzaji bora wa fedha, Gavana Tutuba alisema BoT inashiriki maonesho mbalimbali ambayo yanawafikia wananchi wengi na hupewa elimu hiyo.

> *Kila mwaka tunashiriki maonesho mbalimbali na kule tunaamini tunakutana na watu wengi kutoka kada mbalimbali, miongoni mwa elimu tunazozitoa ni za utunzaji wa fedha, kwa sababu tunaamini kabla ya kuanza kushughulika na adhabu kwa mujibu wa sheria, tunao wajibu wa kumuelimisha mwananchi*
>
> **Gavana Tutuba**

# TISEZA YACHOCHEA UWEKEZAJI MAREKANI, TANZANIA

> *Marekani inaendelea kuwa mdau mkubwa wa maendeleo nchini,ikiwa na jumla ya mtaji wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI Stock) unaokadiriwa kufikia Dola za Marekani bilioni 5.*
>
> ***Bw. Gilead Teri***




Mkurugenzi Mkuu wa TISEZA, Bw. Gilead Teri, akizungumza katika moja ya vikao vya taasisi hiyo.

Wakati biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani ukiendelea kukua kadri miaka inavyoenda, Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (TISEZA) imesaini Hati ya Makubaliano ya Kibiashara na Chama cha Wafanyabiashara wa Marekani (AmCham Tanzania).

Makubaliano hayo yalisainiwa Februari 26, 2026 jijini Dar es Salaam yakiwa na lengo la kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji kati ya nchi hizo pamoja na kupanua wigo wa fursa kwa sekta binafsi za nchi zote mbili.

Akizungumza katika hafla hiyo ya utiaji saini, Mkurugenzi Mkuu wa TISEZA, Bw. Gilead Teri, amesema kuwa Marekani inaendelea kuwa mdau mkubwa wa maendeleo nchini, ikiwa na jumla ya mtaji wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI Stock) unaokadiriwa kufikia Dola za Marekani bilioni 5.

Alieleza kuwa uchumi wa Marekani umejengwa kwa nguvu ya sekta binafsi na mitaji imara, na kwamba matarajio ni kuongeza kiwango hicho cha uwekezaji maradufu ifikapo mwaka 2030.

Aidha, Teri amebainisha kuwa TISEZA imeendeleza majadiliano ya kibiashara yanayolenga matokeo chanya na yenye tija kwa pande zote mbili. Alitoa wito kwa Watanzania wenye mawazo ya kibiashara, miradi iliyofanyiwa upembuzi yakinifu (feasibility studies), na mipango madhubuti ya uwekezaji, kutumia fursa zilizopo kupitia ushirikiano huo mpya.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa AmCham Tanzania, Bw. Geofrey Mchangila, amesema kuwa chama hicho kimejikita katika kuhamasisha uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwemo madini, nishati, afya na kilimo.

Bw. Mchangila aliongeza kuwa makubaliano hayo yanaambatana na uwajibikaji wa pamoja katika kufuatilia utekelezaji wa malengo ya uwekezaji na kupanua wigo wa wawekezaji kutoka Marekani.

Bw. Mchangila amesisitiza kuwa ushirikiano huo pia unaunga mkono Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, inayolenga kukuza Pato la Taifa hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani 7,000 kwa kila Mtanzania.

Akizungumza katika moja ya majukwaa, Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Bi. Elsie Kanza, alisema ongezeko la uwekezaji na biashara kati ya Marekani na Tanzania limetokana na utekelezaji wa mipango kadhaa muhimu, ikiwemo kuanzishwa kwa Tanzania American Chamber of Commerce mwaka 2023.

# FAHAMU BIMA YA AMANA INAVYOKULINDA DHIDI YA HASARA

Mfumo wa bima ya amana ni moja ya nguzo muhimu katika kulinda fedha za wananchi na kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha nchini. Mfumo huu umeanzishwa mahsusi kwa lengo la kuhakikisha kuwa wenye amana hawapotezi fedha zao pale benki au taasisi ya fedha inapofungwa, kufilisika au kufutiwa leseni. Kupitia utaratibu huu, wananchi hupata uhakika wa kurejeshewa fedha zao kwa kiwango kinachokingwa, hali inayowawezesha kuendelea na maisha yao bila kukumbwa na madhara makubwa ya kifedha.

Asili ya mfumo wa bima ya amana ilianza katika nchi zilizoendelea, ambapo kwa mfano, Marekani ilianzisha mfumo huu mwaka 1933 kufuatia changamoto za kifedha zilizokuwa zimeathiri wananchi wengi. Tangu wakati huo, zaidi ya nchi 100 duniani zimeanzisha mifumo rasmi ya kulinda amana za wananchi wao. Tanzania pia imefuata mkondo huo kwa kuanzisha mfumo huu kupitia Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, ambapo utekelezaji wake unasimamiwa na Bodi ya Bima ya Amana (DIB).

Kwa Tanzania, umuhimu wa mfumo huu umeonekana wazi katika kulinda maslahi ya wenye amana pamoja na kuimarisha imani ya umma katika sekta ya fedha. Wananchi wanapokuwa na uhakika kwamba fedha zao ziko salama hata kama taasisi ya fedha itakumbwa na matatizo, huendelea kutumia huduma za kibenki bila hofu. Hali hii pia huchochea ujumuishi wa kifedha kwa kuwahamasisha watu wengi zaidi kujiunga na mfumo rasmi wa fedha.

Moja ya majukumu makuu ya mfumo wa bima ya amana ni kulipa fidia kwa wenye amana wanaostahili pale taasisi ya fedha inaposhindwa kuendelea na shughuli zake. DIB ina jukumu la kuhakikisha kuwa malipo haya yanafanyika kwa wakati na kwa ufanisi ili kupunguza usumbufu kwa wananchi. Kimataifa, inapendekezwa kuwa mfumo madhubuti uweze kulinda angalau asilimia 90 ya wenye amana kwa kiwango cha asilimia 100 ya fedha zao, jambo ambalo Tanzania imefanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Katika kipindi cha zaidi ya miaka 26 iliyopita, Benki Kuu ya Tanzania, ambayo ndiyo mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa sekta ya benki nchini, imekuwa ikiiteua DIB kama mfilisi wa benki na taasisi za fedha zilizofutiwa leseni kwa sababu mbalimbali. Hadi sasa, DIB inaendesha ufilisi wa benki na taasisi za fedha tisa zilizofungwa na Benki Kuu kati ya mwaka 2000 na 2018.

Taasisi hizo zilizo chini ya ufilisi ni: Greenland Bank (T) Limited, Delphis Bank (T) Limited, FBME Bank Limited, Mbinga Community Bank, Njombe Community Bank, Covenant Bank for Women, Efatha Bank, Meru Community Bank na Kagera Farmers' Cooperative Bank. Zoezi la ufilisi katika taasisi hizo linaendelea na liko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Kwa miaka ya hivi karibuni, kiwango cha juu cha kinga ya amana nchini kimeongezwa kwa kiasi kikubwa. Awali kilikuwa shilingi 250,000 mwaka 1994, kikaongezeka hadi 500,000 mwaka 2003, na kufikia shilingi 1,500,000 mwaka 2010. Hata hivyo, kufuatia ukuaji wa sekta ya fedha na mahitaji ya wananchi, mwaka 2023 kiwango hicho kiliongezwa hadi shilingi 7,500,000 kwa kila mwenye amana. Ongezeko hili limewezesha kulinda zaidi ya asilimia 99 ya wenye amana nchini, hatua inayodhihirisha dhamira ya serikali katika kulinda maslahi ya wananchi.

Mbali na kulipa fidia, DIB pia ina jukumu la kusimamia ufilisi wa benki na taasisi za fedha zinazoshindwa kuendelea na shughuli zake. Katika kipindi cha zaidi ya miaka 26 iliyopita, taasisi hii imekuwa ikiteuliwa kusimamia ufilisi wa benki kadhaa zilizofungwa, na kuhakikisha kuwa mali zinakusanywa na kugawiwa kwa haki kwa wadai, wakiwemo wenye amana.

Aidha, jukumu lingine muhimu ni kushiriki katika kutafuta suluhisho la changamoto zinazoweza kuzikumba taasisi za fedha kabla hazijafikia hatua ya kufungwa. Kuanzia Julai 2025, DIB imeanza kushiriki kikamilifu katika hatua za mapema za kupunguza hasara kwa taasisi zinazokumbwa na changamoto. Lengo ni kuzipatia nafasi ya kurejea katika hali ya kawaida badala ya kufungwa kabisa, hatua ambayo mara nyingi huambatana na gharama kubwa zaidi.

Katika kutekeleza majukumu yake, DIB pia hushiriki katika kubaini na kupunguza vihatarishi vinavyoweza kuathiri sekta ya fedha. Hii inahusisha ufuatiliaji wa karibu wa taasisi za fedha pamoja na kushirikiana na wadau wengine muhimu kama Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha. Ushirikiano huu husaidia kuhakikisha kuwa hatua za haraka zinachukuliwa pale dalili za hatari zinapobainika.

Kwa ujumla, bima ya amana ina mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla. Inalinda fedha za wananchi, inaongeza imani katika mfumo wa fedha, na inachochea matumizi ya huduma za kibenki. Faida hizi haziwanufaishi tu wenye amana, bali pia taasisi za fedha na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Kwa msingi huo, ni muhimu kwa wananchi kuendelea kuwa na uelewa wa mfumo huu na kuutumia ipasavyo. Kaulimbiu ya DIB ya "Tunakinga Amana Yako" inaakisi dhamira ya kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata ulinzi wa fedha zake na kuishi kwa uhakika zaidi kifedha.

# TANZANIA YAZINDUA MFUKO WA ETF WA KUWEKEZA KIKANDA




Afisa Mtendaji Mkuu wa CMSA, CPA. Nicodemus Mkama, akizungumza katika uzinduzi wa Mfuko wa ETF wa kuwekeza kikanda uliofanyika Januari 28 2026.

Tanzania imeandika historia mpya katika maendeleo ya masoko ya mitaji baada ya kuzinduliwa na kuorodheshwa kwa mfuko wa kwanza wa uwekezaji wa Exchange Traded Fund (ETF) unaowekeza katika kampuni kubwa za Afrika Mashariki.

Uzinduzi huo ulifanywa kwa ushirikiano wa Mamlaka ya Mitaji ya Masoko na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na iTrust Finance Limited kupitia mfuko ujulikanao kama iTrust EAC Large Cap ETF, ambao umeorodheshwa rasmi DSE.

Mfuko huo ni wa kwanza nchini unaowezesha wawekezaji kununua vipande vya uwekezaji vinavyowapa nafasi ya kuwekeza katika hisa za kampuni kubwa zenye utendaji mzuri zilizoorodheshwa katika masoko ya hisa ya nchi za Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Januari 28, 2026 wakati wa uzinduzi wa mfuko huo, hatua hiyo inaongeza wigo wa bidhaa za uwekezaji nchini na kuimarisha nafasi ya Tanzania katika ramani ya masoko ya mitaji ya kikanda.

Mfuko wa iTrust EAC Large Cap ETF unasimamiwa na iTrust Finance Limited huku Benki ya NBC ikiwa mdhamini wa dhamana wa mfuko huo.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi huo, Mtendaji Mkuu wa CMSA, Nicodemus Mkama, alisema mauzo ya vipande vya mfuko huo yamepata mafanikio makubwa.

Alieleza kuwa takribani asilimia 99.44 ya vipande vilinunuliwa na wawekezaji binafsi huku asilimia 0.56 vikichukuliwa na taasisi mbalimbali za uwekezaji.

"Mafanikio haya yanaonyesha kuwa mazingira ya uwekezaji nchini yanaendelea kuimarika kutokana na sera nzuri za serikali pamoja na mifumo bora ya usimamizi wa masoko ya mitaji," alisema Mkama.

Aliongeza kuwa hatua ya kuanzishwa kwa mfuko huo pia imechangiwa na maboresho ya sera, ikiwa ni pamoja na kupunguza kiwango cha chini cha ushiriki wa wawekezaji kutoka TZS 1,000,000 hadi TZS 100,000 ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kushiriki katika uwekezaji.



Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa DSE, Peter Nalitolela, alisema kuorodheshwa kwa mfuko huo ni hatua muhimu katika kupanua bidhaa za uwekezaji katika soko la hisa nchini.

Naye Mtendaji Mkuu wa iTrust Finance Limited, Faiz Arab, alisema kampuni yake imefurahia kuwa ya kwanza kuanzisha mfuko wa ETF unaowekeza kikanda.

Alisema mfuko huo unalenga kutoa fursa zaidi za uwekezaji zilizo wazi na zenye uwazi mkubwa kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

Wadau wa masoko ya mitaji wanaamini kuwa kuanzishwa kwa mfuko huo kutasaidia kuongeza ukwasi katika soko la hisa la Dar es Salaam na kutoa njia rahisi kwa wawekezaji kuwekeza katika kampuni kubwa za ukanda wa Afrika Mashariki kupitia bidhaa moja ya uwekezaji.



# DKT. MAHFOUDH AHIMIZA HAKI, USAWA, NA UWEZESHAJI WA WANAWAKE




Naibu Gavana wa BoT anayesimamia Utawala na Udhibiti wa Ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh, akitoa hutuba ya ufunguzi wa hafla ya maadhimisho ya Siku ya Wananwake Duniani, iliyofanyika Machi 27, 2026, Makao makuu ndogo ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam.

Naibu Gavana, Utawala na Udhibiti wa ndani, Dkt. Rahma Mahfoudh, amehimiza uwepo wa haki, usawa, na uwezeshaji wa wanawake ndani ya Benki Kuu na Taifa kwa ujumla ili kuweza kufikia maendeleo jumuishi.

Dkt. Mahfoudh aliyasema hayo kwenye hafla ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, iliyofanyika Machi 27, 2026 Makao Makuu ndogo ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Dar es Salaam.

Alisema kuwa ni wakati wa kuchukua hatua za vitendo kwani maendeleo jumuishi hayawezekani bila ushiriki kamili wa wanawake katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi, akihimiza kuwepo kwa mazingira yanayowawezesha wanawake kufikia fursa sawa katika ajira, mafunzo, na nafasi za uongozi.

Katika hotuba hiyo, aliwapongeza wanawake wa Benki Kuu kwa mchango wao mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi na katika maendeleo ya uchumi wa taifa.

Aidha, alibainisha kuwa wanawake hao wamejidhihirisha kuwa nguzo imara, si tu katika utendaji kazi, bali pia katika kujitolea kwa jamii kupitia misaada na ushirikiano na makundi yenye uhitaji.

"Pamoja na mafanikio yote, lakini kuna umuhimu wa wanawake kutumia kikamilifu fursa zilizopo kwa ajili ya maendeleo yao binafsi na kitaaluma. Rai yangu kwenu muendelee kujiamini, kuthubutu, na kuacha hofu au mashaka yanayoweza kuzuia kufikia malengo yenu,"alisema Dkt. Mahfoudh

Pia, Naibu Gavana alihimiza umuhimu wa ushirikiano kati ya wanawake na uongozi wa taasisi katika kubaini na kuondoa vikwazo vya kisera, taratibu au mazingira ya kazi vinavyokwamisha maendeleo ya wanawake.


"Vilevile, kila mwanamke anapaswa kuwa balozi wa haki na usawa kwa vitendo, kwa kuhakikisha anathamini na kutoa fursa kwa wengine bila ubaguzi,"aliongeza

Dkt. Mahfoudh alihitimisha kwa kutoa wito wa mshikamano na uwajibikaji wa pamoja katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo 2050, akisisitiza juhudi za pamoja ili kuweza kuleta mabadiliko.

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2026 yameongozwa na kauli mbiu "Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana: Msingi Jumuishi Kufikia Dira 2050."






Gavana Emmanuel Tutuba, akizungumza katika hafla ya futari iliyofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 6 Machi 2026.

# GAVANA BOT; TUDUMISHE AMANI KUIMARISHA UCHUMI WETU

Katika kuadhimisha mwezi mtukufu wa Ramadhani, Benki kuu ya Tanzania (BoT) iliandaa hafla maalum ya futari jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya kuimarisha uhusiano na wadau wake.

Hafla hiyo iliyofanyika Machi 6, 2026 ilihudhuriwa na viongozi wa dini, serikali, mabenki na taasisi za fedha nchini pamoja na watu wenye mahitaji maalumu.

Akizungumza katika hafla hiyo, Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba amewataka watanzania wote kudumisha amani, uzalendo na ushirikiano katika kujenga uchumi wa Tanzania.

"Naomba tuendelee kuliombea taifa letu amani, upendo na mshikamano. Tuendelee kudumisha uzalendo na ushirikiano katika kujenga uchumi wetu, hasa katika kipindi hiki ambacho uchumi wa dunia unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mivutano ya kisiasa na misukosuko ya kiuchumi,"

Pia, katika hafla hiyo Gavana aliwaeleza washiriki kuwa uchumi umeendelea kuimarika, sekta ya fedha iko imara, yenye mtaji na ukwasi wa kutosha, inayojiendesha kwa ufanisi na faida, na inayokua kwa kasi ya kuridhisha.

"Mwaka 2025, uchumi wa Tanzania ulikua kwa takriban asilimia 6, huku Zanzibar uchumi ukikua kwa asilimia 6.8. Mwaka 2026, ukuaji unatarajiwa kufikia asilimia 6.3 kwa Tanzania Bara na asilimia 7.2 kwa Zanzibar.", alieleza Gavana huyo.

Alisema kuwa ukuaji huo wa uchumi umechochewa na kuimarika kwa shughuli za kilimo, upatikanaji wa umeme wa uhakika, mazingira bora ya biashara, kuongezeka kwa mauzo ya nje hususan dhahabu na kahawa, pamoja na ongezeko la watalii nchini.

Aliongeza kuwa sekta ya benki imeendelea kuwa thabiti, ikiwa na ukwasi wa kutosha kuwezesha utoaji wa mikopo na mtaji wa kuhimili misukosuko ya kiuchumi pamoja na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu hadi kufikia asilimia 2.8 mwaka 2025 ambayo ni chini ya ukomo unaokubalika wa asilimia 5.

Awali, Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Dkt. Abubakar Zubeir alipongeza Benki Kuu kwa kuandaa hafla hiyo akiitaja kuwa ni ishara tosha kwamba BoT inathamini umoja na inaamini katika kuwaleta Watanzania pamoja bila kujali tofauti za kidini au kijamii.

"Hatua hii ya Benki Kuu ya Tanzania inaonyesha kuwa katika taifa letu hakuna ubaguzi; sisi sote ni Watanzania, tunashirikiana kujenga nchi yetu, na tunapaswa kuendelea kuimarisha mshikamano huo kwa manufaa ya taifa letu". Alisema Mkurugenzi wa Mambo ya Nje wa Baraza Kuu la waislamu Tanzania (Bakwata), Sheikh Sharif Tahir Almusawa kwa niaba ya mufti Dkt Zubeir.



Gavana Emmanuel Tutuba, akizungumza katika hafla ya futari iliyofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 6 Machi 2026.

# MATAWI YA BENKI KUU YAFUTURISHA WENYE UHITAJI

Katika kuendelea kudumisha ushirikiano na jamii inayoizunguka, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Machi 6, 2026 iliandaa futari maalumu kwa ajili ya watu wenye uhitaji pamoja na wafanyakazi wake katika matawi mbalimbali nchini.

Futari ya kitaifa ya BoT ilifanyika katika Makao Makuu Ndogo jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, viongozi wa dini, viongozi wa Serikali pamoja na watu wenye uhitaji.

Akizungumza katika hafla hiyo, Gavana Tutuba aliwataka Watanzania kuendelea kudumisha amani, uzalendo na ushirikiano ili kuimarisha uchumi wa taifa.

Mbali na hafla hiyo ya kitaifa kufanyika Dar es Salaam, Gavana Tutuba pia aliandaa futari katika matawi yote ya BoT nchini, yakiwamo Dodoma, Zanzibar, Arusha, Mbeya, Mwanza na Mtwara ambapo yalijumuika na watu wenye uhitaji wakiwamo Watoto yatima.

## *Dodoma*

Katika Tawi la Dodoma, mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, ambaye aliipongeza BoT kwa kuendelea kuikumbuka jamii inayozunguka taasisi hiyo, hususan watu wenye uhitaji.

Katika hafla hiyo, tawi hilo lilialika vituo vitatu vya watoto yatima kushiriki futari hiyo pamoja.




**Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule akizungumza katika hafla ya iftar iliyoandaliwa na Benki Kuu Tawi la Dodoma.**

## *Mwanza*

Hafla hiyo pia ilifanyika katika Jiji la Mwanza, ambapo BoT Tawi la Mwanza lilimualika Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Bw. Said Mtanda, kuwa mgeni rasmi.



**Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda (katikati) pamoja na Naibu Gavana wa BoT, Dkt. Yamungu Kayandabila wakikabidhi mahitaji kwa mlezi wa kituo cha watoto yatima mkoani Mwanza.**

## *Zanzibar*

BoT Tawi la Zanzibar lilimualika Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Dkt. Juma Malik Akil, kuwa mgeni rasmi.



**Waziri wa Fedha na Mipango, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil akishiriki katika hafla ya Iftar iliyoandaliwa na BoT Zanzibar.**

# MATAWI YA BENKI KUU YAFUTURISHA WENYE UHITAJI

## *Mtwara*

Kwa upande wa Tawi la BoT Mtwara, mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Bw. Abdallah Mwaipaya, ambaye aliipongeza BoT kwa kuendelea kuwa karibu na jamii na kuwakumbuka watu wenye uhitaji.



**Mkuu wa Wilaya ya Mtwara mjini, Mhe. Abdallah Mwaipaya (katikati waliokaa) katika picha ya pamoja na viongozi wa BoT Tawi la Mtwara na viongozi wa dini.**

## *Arusha*

Katika Tawi la Arusha, lilimualika Mkuu wa Wilaya ya Arusha kuwa mgeni rasmi ambaye aliwakilishwa na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Bw. Jacob Rombo.



**Meneja wa Idara ya Uchumi wa BoT Tawi la Arusha, Aristedes Mrema akizungumza kwa niaba ya mkurugenzi wa tawi hilo katika hafla ya iftar.**

## *Mbeya*

Nalo Tawi la BoT Mbeya liliandaa futari hiyo ambapo mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Bi. Josephine Manase, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Bw. Beno Malisa.

Hatua ya BoT kuandaa futari pamoja na watu wenye uhitaji ni sehemu ya juhudi za taasisi hiyo za kuimarisha mahusiano na jamii inayoizunguka pamoja na kudumisha mshikamano na ushirikiano katika jamii kwa ujumla.



**Mkurugenzi wa BoT Tawi la Mbeya, Dkt. James Machemba akikabidhi msaada kwa mlezi wa kituo cha watoto wenye uhitaji mkoani humo.**

# BOT YAWANOA WAANDISHI WA HABARI ZA UCHUMI KIGOMA





Mchambuzi wa Masuala ya Fedha kutoka Kurugenzi ya Masoko ya Fedha, Bw. Ephraim Madembwe akitoa wasilisho katika mafunzo hayo.



Meneja Msaidizi wa Uhusiano wa Umma BoT, Bi. Noves Moses akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Meneja wa Mawasiliano, Bi. Victoria Msina.



Afisa wa Benki Kuu kutoka Kurugenzi ya Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha, Bw. Bondo Kafuku akitoa wasilisho kwa waandishi wa habari mkoani Kigoma wakati wa mafunzo hayo.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iliendesha mafunzo ya siku mbili kwa waandishi wa habari za uchumi na biashara kutoka Kanda ya Magharibi, kwa lengo la kuongeza uelewa na umahiri wao katika kuripoti kwa usahihi masuala yanayohusu shughuli na majukumu ya Benki Kuu.

Mafunzo hayo yalifanyika mkoani Kigoma kuanzia tarehe 26 hadi 27 Februari 2026 na kuwashirikisha jumla ya waandishi wa habari 35 kutoka mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora na Kagera.

Akisoma hotuba ya ufunguzi kwa niaba ya Meneja wa Mawasiliano wa BoT, Bi. Victoria Msina, Meneja Msaidizi wa Uhusiano wa Umma, Bi. Noves Moses, alisema kuwa semina hizo zinalenga kuimarisha ubora na usahihi wa uripotiji wa habari zinazohusu Benki Kuu na mchango wake katika uchumi wa taifa.

Aidha, Bi. Noves alibainisha kuwa mwaka huu BoT inaadhimisha miaka 60 tangu kuanzishwa kwake, na kwamba maadhimisho hayo ni fursa kwa waandishi wa habari kuandika makala zinazoangazia mchango wa Benki Kuu katika ukuaji wa uchumi pamoja na kuenzi kazi inayofanywa na BoT katika kusimamia uthabiti wa uchumi wa nchi.

Miongoni mwa mada zilizowasilishwa katika semina hiyo ni: Majukumu ya Benki Kuu na utekelezaji wa Sera ya Fedha ikiwemo Riba ya Benki Kuu; umuhimu wa ununuzi wa dhahabu na faida zake katika kuimarisha akiba ya taifa; usimamizi wa mifumo ya malipo ya taifa; utambuzi wa alama za usalama katika noti; pamoja na namna BoT inavyopokea na kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za fedha.



# WENYE MAHITAJI MAALUM DODOMA WANUFAIKA MAFUNZO YA BOT

Afisa wa Benki Kuu kutoka Idara ya Operesheni BoT Tawi la Dodoma, Bw. Atufigwege Mwakabalula akitoa wasilisho kwa walemavu wilayani Chemba mkoani Dodoma.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ikiwa inaendeleza azma ya kutoa elimu jumuishi ya fedha kwa Watanzania, imetoa mafunzo maalumu kwa watu wenye ulemavu kuhusu utambuzi wa alama za usalama katika noti.

Mafunzo hayo yalitolewa Alhamisi, Machi 19, 2026, wilayani Chemba mkoani Dodoma, yakihusisha walemavu wa kusikia pamoja na wasioona, kwa lengo la kuwawezesha kutambua fedha halali na kujikinga dhidi ya utapeli.

Akizungumza kwa niaba ya Meneja wa Mawasiliano wa BoT, Afisa Mwandamizi kutoka Idara ya Mawasiliano, Bw. Sadi Makomba, amesema kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya juhudi za Benki Kuu kuhakikisha kuwa hakuna kundi linaloachwa nyuma katika upatikanaji wa elimu ya fedha.

"Lengo la Benki Kuu ni kumjumuisha kila mwananchi katika elimu ya fedha, hususan makundi maalumu. Makundi haya hukumbana na changamoto ya kutambua fedha halali na hivyo kujikuta katika matatizo kutokana na ukosefu wa elimu sahihi," alisema Bw. Makomba.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Shirika la Walemavu Mkoa wa Dodoma, Bw. Omary Lubuva, aliishukuru BoT kwa kutoa mafunzo hayo, akieleza kuwa yameziba pengo kubwa la ukosefu wa elimu ya fedha kwa kundi la walemavu wilayani Chemba.

Alisema hatua hiyo ni muhimu katika kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kujikinga na udanganyifu unaohusiana na fedha.

Hatua ya BoT inaonesha dhamira ya dhati ya kulitambua na kulijumuisha kundi la watu wenye ulemavu katika masuala ya kifedha, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 inayolenga kujenga uchumi imara na shindani.



Mwenyekiti wa Chama cha Walemavu Mkoa wa Dodoma, Bw. Omary Lubuva akizungumza katika mafunzo hayo yaliyofanyika wilayani Chemba.





# BOT MGUU SAWA KUADHIMISHA MIAKA 60 KWA KISHINDO

Ni kishindo cha Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kauli hii inaakisi uimara na umuhimu wa taasisi hii nyeti nchini katika kusimamia uchumi imara na jumuishi inapotimiza miaka 60 mwaka huu.

Maadhimisho hayo yanatarajiwa kufanyika Juni 2026 ikiwa ni kumbukumbu ya kuanzishwa rasmi kwa taasisi hiyo Juni 14, 1966, hatua iliyokuja baada ya mageuzi muhimu katika mfumo wa kifedha nchini.

Kabla ya kuanzishwa kwa BoT, shughuli za kifedha nchini zilisimamiwa na Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (EACB), ambayo ilikuwa inahudumia nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika, huku Zanzibar ikijiunga baadaye. Bodi hiyo ilisimamia utoaji wa sarafu ya Shilingi ya Afrika Mashariki, kufanya malipo, kusimamia sera ya fedha na ubadilishanaji wa fedha za kigeni, pamoja na kuwa kama benki ya mabenki.

Mfumo huu uliendeshwa kwa kufuata sera za Uingereza, hasa kutokana na shilingi hiyo kufungamanishwa na Paundi ya Uingereza, hali iliyosababisha Tanzania kukosa uhuru kamili wa kusimamia sera zake za fedha.

Hali ilibadilika rasmi Juni 14, 1966, baada ya kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Tanzania chini ya Sheria ya mwaka 1965, ikiwa na jukumu la kusimamia sera za fedha kwa manufaa ya taifa. Tangu wakati huo, BoT imekuwa mhimili mkuu wa uchumi kwa kutekeleza majukumu kama kutoa sarafu ya taifa, kuwa benki ya serikali, benki ya mabenki, kudhibiti mikopo, kuwa mkopeshaji wa mwisho na kusimamia benki pamoja na taasisi za fedha.

Katika miaka yake ya mwanzo (1966 –1967), BoT ilitumia zaidi zana zisizo za moja kwa moja za sera ya fedha, sambamba na mfumo wa uchumi wa soko uliorithiwa kutoka kipindi cha ukoloni.

Akizungumza kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya miaka 60, Meneja wa Idara ya Mawasiliano wa BoT, Bi. Victoria Msina, alisema tukio hilo litakuwa fursa ya kutathmini mchango wa benki hiyo katika kuimarisha uchumi wa taifa kwa kipindi cha miongo sita. Alieleza kuwa maadhimisho hayo yanalenga kuangazia mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa BoT, hususan katika kusimamia sera ya fedha, kudhibiti mfumuko wa bei na kudumisha uthabiti wa uchumi wa nchi.

Katika hatua ya sasa, BoT imepanua wigo wa majukumu yake ili kuendana na mahitaji ya uchumi wa kisasa. Mbali na majukumu ya msingi, sasa inajihusisha kikamilifu na kusimamia uthabiti wa mfumo wa fedha, kudhibiti mfumuko wa bei, kusimamia mifumo ya malipo ya kidijitali kama mobile money, pamoja na kuimarisha ujumuishwaji wa kifedha kwa wananchi.

Aidha, benki hiyo imeendelea kushirikiana na taasisi za kimataifa na wadau wa maendeleo katika kuimarisha sera za fedha na uchumi. Maadhimisho hayo pia yatahusisha shughuli mbalimbali zikiwemo mikutano ya kikanda, maonesho ya elimu kwa umma na programu za kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya fedha na uchumi. Kupitia majukwaa ya kidijitali na vyombo vya habari, BoT inalenga kuwafikia wananchi wengi zaidi na kuwajengea uwezo wa kifedha.

Bi. Msina aliongeza kuwa pamoja na mafanikio ambayo taasisi hiyo imeyapata katika kipindi cha miongo sita iliyopita, maadhimisho hayo, ambayo yatakuwa na matukio mbalimbali, yatatathmini changamoto ambazo zimejitokeza katika kipindi na namna ambavyo zimetatuliwa, pamoja na uelekeo wa Benki Kuu katika miaka ijayo.

"Maadhimisho hayo pia yatatumika kuimarisha ushirikiano kati ya BoT na wadau mbalimbali wa sekta ya fedha, wakiwemo benki kuu kutoka katika kanda za Mashariki na SADC, benki za biashara, taasisi za fedha, Serikali na wadau wengine wa maendeleo,"alisema Bi. Msina

Kwa mujibu wa Bi. Msina, katika kipindi cha maadhimisho hayo kutafanyika shughuli mbalimbali kwa takribani wiki nzima, zikiwemo mikutano na vikao vya kikanda vitakavyowakutanisha watendaji wakuu wa benki kuu kutoka Afrika Mashariki na nchi nyingine za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Viongozi hao watajadili masuala ya sekta ya fedha na maendeleo ya uchumi kwa ujumla.

Mbali na mikutano hiyo, BoT pia itafanya maonesho maalumu yatakayowapa wananchi na wadau fursa ya kujifunza kuhusu majukumu, shughuli na mafanikio ya taasisi hiyo kupitia kurugenzi na idara zake mbalimbali.

Katika hatua nyingine, Bi. Msina alisema maadhimisho hayo yatahusisha wadau wa sekta ya fedha pamoja na wananchi kupitia majukwaa mbalimbali ya mawasiliano, ikiwemo mikutano ya wadau na programu za elimu ya fedha kwa umma. Alisema BoT pia itatumia vyombo vya habari na majukwaa ya kidijitali kuwafikia wananchi wengi zaidi ili kuongeza uelewa wa masuala ya fedha na uchumi.

"Kama tutakavyoona, maadhimisho haya si sherehe tu, bali pia ni fursa ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya fedha na uchumi," alisema.

Alifafanua kuwa elimu hiyo itatolewa kupitia mitandao ya kijamii ya Benki Kuu ikiwemo Instagram, Facebook na WhatsApp Channel, pamoja na kushirikiana na waandishi wa habari kupitia programu za ziara kwenye vyombo vya habari (media tours) ambazo zitasaidia kuelezea mchango wa BoT katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Aidha, maonesho ya elimu kwa umma yatatumika kutoa ufafanuzi kuhusu shughuli zinazotekelezwa na idara na kurugenzi mbalimbali za BoT.

"Maadhimisho ya miaka 60 ya BoT yanatarajiwa kuwa jukwaa muhimu la kuangazia historia ya taasisi hii, kuimarisha ushirikiano na wadau wa sekta ya fedha pamoja na kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya fedha na uchumi nchini,"alisema Meneja huyo wa Mawasiliano wa BoT.

# ELIMU YA NOTI YAWAFIKIA VIZIWI WILAYANI KYELA



Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kupitia Tawi lake la Mbeya, imetoa elimu ya fedha kwa watu wenye ulemavu wa kusikia (viziwi) wilayani Kyela, mkoani Mbeya, kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kutambua alama za usalama katika noti pamoja na umuhimu wa utunzaji sahihi wa fedha.

Elimu hiyo ilitolewa katika semina maalum iliyoandaliwa kwa ushirikiano na Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMIVITA), ikiwa ni sehemu ya juhudi za BoT kuhakikisha makundi yote katika jamii yanapata uelewa wa kutosha kuhusu matumizi sahihi ya fedha na utambuzi wa noti halali.

Akifungua semina hiyo tarehe 17 Machi 2026, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Mhe. Josephine Manase, aliipongeza Benki Kuu ya Tanzania kwa kuendelea kuwafikia makundi maalum, akisisitiza kuwa elimu hiyo ni muhimu katika kulinda jamii dhidi ya matumizi ya fedha bandia na kuimarisha ujumuishwaji wa kifedha.

Washiriki wa semina hiyo walipata fursa ya kujifunza kwa vitendo kuhusu sifa kuu za noti halali za Tanzania pamoja na mbinu bora za kuzitunza ili kudumisha ubora na uhalali wake.



# MIFUMO YA MALIPO, HUDUMA ZINAENEA

Uchumi kuimarisha, pia wigo wa huduma,
Hali inafurahisha, Tanzania tunasema,,
Matokeo yaonyesha, kwamba sisi tuko vema,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

BoT Naibu Gavana, Msemo ndiye kasema,
Maendeleo twaona, kupatikana huduma
Ni za fedha twaziona, kila kona zinasoma,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

Kama wataka kulipa, rahisi sana nasema,
Kwa TIPS ulipo lipa, muamala utasoma,
Tena kwa kasi mara pa, umekamilisha vema,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

Nchini maendeleo, hata wengine wasema,
Tumefikia upeo, katika kanda twavuma,
Hiki pia kichocheo, uchumi kufanya vema,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

Mzuri usimamizi, mifumo weze simama,
Tukifanya matumizi, wala kusiwe na noma,
Hii njema sana kazi, zinasambaa huduma,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

Miamala bigi TISS, kupokea na kutuma,
TACH malipo halisi, madogo tunajituma,
Papo kwa hapo ni TIPS, huu sana umevuma,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

Hata kwa nia za simu, huduma fedha twasema,
Mitandao ni muhimu, kotekote wanasema,
Wengi wenye ufahamu, walipa wamesimama,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

Kama kuhamisha pesa, yapatikana huduma,
Kwa simu na benki hasa, yote yafanyika vema,
Hii ni kubwa hamasa, vema sana kuisema,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

Na Afrika Mashariki, EAPS ndiyo yavuma,'
Sarafu zetu zatiki, huku na huko kutuma,
Na kote wameafiki, mfumo ulivyo mwema,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

Mifumo kusimamia, kanda yetu jambo jema,
Tuweze kuitumia, vizuri bila kukwama,
Izidi kusaidia, nchi zetu wanachama,
Kwa mifumo ya malipo, huduma zinaenea.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**

**Limetolewa na Idara ya Mawasiliano**
**Benki Kuu ya Tanzania**

Anuani:
**Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete, 40184**
**S.L.P. 2303 Dodoma, Tanzania**
Barua pepe:
**botcommunications@bot.go.tz**
**info@bot.go.tz**
Tovuti:
**www.bot.go.tz**